**Jiko** la mkaa ladaiwa chanzo kifo cha mpigadebe, abiria

UKURASA 3



**Majaliwa** aiongezea muda kamati ya moto wa Kariakoo

UKURASA 3

**ama**

ALHAMISI JULAI 22, 2021 | AFYA NA MAZINGIRA



MATUNDA YA JUHUDI ZA MIAKA 70

WHO yaitangaza rasmi China haina malaria



JESHI ZIMAMOTO NA UOKOAJI

'Tumekwama maji sakata linaloitesa vita vya moto tangu miaka ya 1970'

KUTOKA FEDHA ZA RAIS SAMIA...

**Waziri atabasamu matumizi shilingi bilioni 9.2 Hospitali ya Wazazi Meta**

•Hospitali Mkoa yaleyale, DC aishikia 'bango'



UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580649

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Chanjo 2 corona zaletwa Tanzania

UK. 2

**Rais** Mwinyi naye athibitisha Zanzibar... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika Baraza la Eid El Adha lililofanyika kitaifa kwenye Msikiti wa Mtoro, Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

## Samaki waliokufa wazagaa ufukweni

UKURASA 4

## Mbowe 'achomolewa' hotelini usiku mnene

UK. 2


**MICHEZO** | **SIMBA YATAMBA IMEPATA 'DAWA'** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaji Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akifuatilia kwa makini hotuba ya swala ya Eid El Adha, katika Msikiti wa Mwitani Wete, Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali: Chanjo 2 corona zipo nchini

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema chanjo zimefika nchini na anayehitaji kuchanjwa yupo huru kuchanjwa wakati wowote katika hospitali maalumu kwa huduma hiyo.

Amesema serikali ilichukua uamuzi wa busara wa kuagiza na kuziletea chanjo nchini baada ya kugundua kuna Watanzania ambao ni wafanyabiashara na wasafiri wa shughuli tofauti nje ya nchi, ambazo sharti upatiwe au kuwa na cheti cha chanjo kuingia nchini mwao.

Waziri Mkuu pia amesema jamii izingatie lishe na mfumo uliotumika mwaka jana katika kuimarisha kinga kwa kula malimao pamoja na matunda uendelee kupambana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Majaliwa ametoa wito huo jana katika Baraza la Eid El Hajj, lililofanyika katika Msikiti wa Mtoro, Ilala jijini Dar es Salaam huku akisisitiza kila Mtanzania kuliombea taifa ili kujinusuru na ugonjwa huo ulioathiri zaidi mataifa mengine.

"Chanjo ipo, anayetaka akachanje, hospitali zimeelezwa mahali zilipo, nenda, ni kinga pia. Juzi nikiwa Morocco, hii ni nchi rafiki na Tanzania, lazima uwe umepima mara kadhaa, vipimo vikionyesha upo vizuri, sawa.

"Katika salamu za Eid nilisema hili, muhimu kwa Watanzania. Kuna Watanzania ambao wanataka kwenda huko wakatimize haja zao, tukaona utafiti ufanyike ili kuona wenzetu wamechanja ipi, ambayo haina madhara kwa kiasi kikubwa... tukabaini ipi nzuri tumepata mbili kati ya zote.

"Kuna Watanzania walikwenda hata Afrika Kusini kuchanja. Tumezileta nchini kila anayehitaji apate fursa ya kuchanjwa, badala ya kufanya mtu aende nje ya nchi," alisema.

Majaliwa alisema pamoja na kuimarishwa mahitaji kwa mahitaji muhimu ya kupambana ugonjwa huo katika maeneo tofauti ikiwamo mipakani, alisisitiza kila mmoja kuchukua tahadhari ili kukabiliana na corona.

"Nchi zetu za jirani zinakabiliwa na ugonjwa huu sana kuliko sisi, hatujazuia mipaka ili kuruhusu kila mmoja na Watanzania kujitafutia riziki, wapo tunaowatambua baada ya kuchunguzwa maeneo fulani, lakini wapo walioambukizwa na corona na hatujawatambua.

"Tufuate kanuni kwa kuendelea kunawa mikono, hapa msikitini nimeona kabla ya kuingia tunanawa mikono, ila tuongeze sabuni mimininka kabla ya kuingia msikitini tuchukue tahadhari.

"Waislamu hatujamudu kwenda Makka, kwa ajili ya hija, wenyeji wetu wamesema hapana, nchi chache ambao wao waamini walijizatiti kwa chanjo walikwenda, bado kuna maambukizi, watu wake ambao wana chanjo.

"Ukijua upo chini ya mita moja kutoka kwa mwenzako, ukiingia msikitini, vaa barakoa. Ugonjwa huu huwapata zaidi walio na miaka 45 na kuendelea.

"Tuzingatie yanayopunguza maambukizi, kufanya mazoezi ili utoke jasho, kwa kutembea umbali mrefu afya inapokuruhusu, mazoezi hata kuzunguka nyumba yako yanatosha," alisema.

Majaliwa pia alitoa rai kwa viongozi wa dini na waumini waendelee kuvumiliana, kustahimiliana na kushikamana na kufanya ibada, kuienzi tunu ya amani bila kujali itikadi za dini na kwamba Tanzania imekuwa nchi kimbilio la waliokosa amani kwa kuwa ina amani.

"Tuendelee kufanya ibada, kuwaombea wenzetu waliotangulia mbele za haki, tuonyeshane upendo na mshikamano hata baada ya kumalizika kwa siku 10 bora ya Dhul Hijja.

"Kila Mtanzania anao mchango mkubwa katika kutunza na kuimarisha amani ya nchi, hivyo wananchi wote tuendelee kuitunza tunu hiyo," alihimiza.

Mufti wa Tanzania, Sheikh Aboubakar Zubeir Bin Ally, aliwataka Watanzania kuendelea kuimarisha maadili mema.

"Tumwombe Mwenyezi Mungu ili tuondokane na majanga yanayoikabili nchi yetu na dunia nzima," alisema na kuwataka waumini wa Kiislamu na watu wote kwa ujumla kufuata mafunzo ya dini yanayotilia mkazo maadili mema na mshikamano.

"Taifa lolote likiwa halina maadili lazima litaporomoka, taifa lolote ni tabia tu, tabia nzuri litaendelea, Watanzania tukiendeleza kudumisha maadili mazuri, tutastawi na kuendeleza nchi yetu," alisema.

# Mbowe 'achomolewa' hoteli usiku mnene

**Na Richard Makore,** MWANZA

NI takribani saa 26 za kilichoonekana kama sinema ya kivita jijini Mwanza, ikianzia muda ambao Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kutangaza kufanya kongamano la kudai Katiba Mpya hadi kukamatwa kwake jana usiku wa manane.

Chimbuko la kukamatwa kwa kiongozi huyo ni mkutano wake na waandishi wa habari wa Jumatatu majira ya saa sita mchana, alipotangaza kufanyika kongamano hilo jijini Mwanza siku ya Jumatano, yaani jana kwa kile alichodai kujikinga dhidi ya corona.

Kabla ya kufanyika kwa kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Robert Gabriel, alitangaza juzi kuzuia mikusanyiko yote, isipokuwa ya kidini, mkoani Mwanza na ilipotimu majira ya saa nane usiku wa kuamkia jana, viongozi mbalimbali wa CHADEMA, akiwamo Mbowe, walikamatwa na Jeshi la Polisi.

Nipashe ilishuhudia jana kipande cha barabara ya lami cha mita takribani 200 kati ya Kona ya Bwiru na Kitangiri kilifungwa na Jeshi la Polisi kwa utepe wa njano kuanzia majira ya saa 12 asubuhi.

Baada ya kufungwa kwa barabara hiyo, hakuna mtu aliyeruhusiwa kukatiza eneo hilo, askari polisi wenye bundi, mabomu ya machozi, mbwa wa polisi na magari ya maji ya kuwasha wakionekana kulidhibiti eneo hilo.

Kwenye eneo ambalo uongozi wa CHADEMA uliliandaa kwa ajili ya mkutano, ukilipia Sh. milioni 1.5, hakukuonekana mwanachama yeyote wa chama hicho.

Nipashe ilishuhudia ukumbi huo ukiwa umepambwa kwa vitambaa vyeupe, bluu na vyekundu, rangi zilizo kwenye bendera ya CHADEMA, huku askari polisi wakiwa wametanda katika hoteli hiyo.

Askari polisi walionekana kumhoji kila aliyetaka kupita kwenye eneo hilo huku wakiwakamata baadhi ya watu waliohisi walikuwa wanataka kuhudhuria kongamano hilo.

Kwenye hoteli aliyofikia Mbowe,

mlinzi wake aliliambia Nipashe kwamba Mbowe alichukuliwa na askari wenye sare majira ya saa nane usiku wa kuamkia jana.

Alidai kuwa kabla ya kukamatwa kwa Mbowe, askari hao walianza kwa kuwakamata watu wengine katika hoteli hiyo ambao hakuwajua kwa majina.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema jana kuwa kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho kinatarajiwa leo mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili hatima ya viongozi wao waliokamatwa mkoani Mwanza wakati wanajiandaa kwa kongamano hilo la kudai Katiba Mpya.

Alisema kikao hicho ni mahususi kwa ajili ya kujua hatima ya viongozi hao ambao walishikiliwa kuanzia usiku wa kuamkia jana mkoani Mwanza kwa kuwa mpaka sasa hawajajua wapo wapi na katika hali gani, lakini wana taarifa kwamba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.

"Jitihada zetu za kumtafuta Mbowe mpaka muda huu (jana mchana) hazijaweza kuthibitisha yupo wapi na yupo katika hali gani.

"Tunatambua kwamba Jeshi la Polisi kupitia kwa msemaji wake mmoja wapo limethibitisha kwenye chombo kimojawapo cha habari kwamba linashikilia watu 11 kwa kile ambacho wamekiita mkusanyiko usio halali lakini hawajataja majina ya hao wanaowashikilia," alisema.

Mbali na Mbowe, viongozi wengine wa CHADEMA waliokamatwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la chama hicho (BAVICHA), John Pambalu.

KAULI YA POLISI

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alipoulizwa kuhusu kuwashikilia Mbowe na wenzake jana, alijibu kwa kifupi kuwa atalitolea maelezo kwa kuwa kwa wakati huo alikuwa kwenye kikao.

Alipotafutwa baadaye jioni, alijibu akisema: "Jeshi la Polisi linasimamia sheria, mwanasiasa ama chama kinachotaka kufanya mikutano ya siasa ni lazima wafuate sheria."

***Imeandaliwa na Richard Makore (MWANZA) na Enock Charles (DAR)**

HABARI KITAIFA

# Rais Mwinyi: Zanzibar ilishachanja mahujaji

**Na Rahma Suleiman,** Z'BAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali ya Zanzibar ilishapokea chanjo ya corona kwa ajili ya mahujaji waliotarajiwa kwenda Makka kuhiji, lakini Serikali ya Saud Arabia imesitisha kupokea wageni kutoka mataifa ya nje kwenda kufanya ibada kwa ajili ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema kuwa kama si Saudia kusitisha kupokea wageni mahujaji kutoka Zanzibar waliotaka kwenda kwenye ibada hiyo wangepata chanjo ya corona.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo wakati akiwahutubia wananchi na Waislamu katika Baraza la Eid Al Adhaa huko katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete Pemba.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa tayari imekamilisha masharti yote yaliyotakiwa kutekelezwa na Serikali ya Sauda Arabia kwa mahujaji watarajiwa kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilishachukua juhudi za kuhakikisha wananchi wake wanatekeleza wajibu huo wa kwenda kuhiji Makka kwa kutafuta chanjo kwa wale ambao walidhamiria kufanya hivyo, lakini kufuatia tamko la Saudia waumini hawakuweza kwenda kutekeleza.

Dk. Mwinyi aliwataka waumini kuwa na subira na kuupokea mtihani huo na wale ambao walitoa pesa zao kwa ajili ya ibada hiyo wajue kuwa pesa zao zitakuwa salama.

Aliyashukuru mataifa yote yaliosaidia kuipatia chanjo Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya matayarisho ya wananchi wake ambao walikuwa na nia ya kwenda kutekeleza ibada hiyo muhimu.

Alisema katika kujenga mikakati na malengo hayo, serikali inakusudia kuufanyia ukarabati mkubwa wa uwanja wa ndege wa Pemba pamoja na bandari ya Mkoani na barabara zinazokwenda katika maeneo huru ya uchumi na uwekezaji.

# Abiria, mpigadebe wafia chumbani kisa jiko mkaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wawili Benitho Mbatha (23), mpigadebe mkazi wa Njombe mjini na Jazila Said (27), mkazi wa Namtumbo mkoani Ruvuma wamefariki dunia baada ya kuingia na jiko la mkaa ndani ya chumba cha kulala.

Tukio hilo lilitokea mkoani Njombe, huku ikielezwa kwamba, waliingia chumbani na jiko kwa lengo la kupunguza baridi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo lilitokea Julai 17, majira ya usiku katika Mtaa wa National Housing Kata ya Njombe Mjini, wakiwa wamelala kwenye chumba kimoja.

"Baada ya kufariki hakuna mtu ambaye aligundua kama kuna watu wamefariki humo ndani," alisema Kamanda Issah.

Aidha alisema: "Sababu ya kifo chao inaonyesha wakati wakiwa hai waliweka moto wa mkaa kwa ajili ya kujihifadhi na baridi, na huu mtindo wa kuweka mkaa kwa watu wa Njombe ndio mtindo wao."

Alitoa wito kwa wananchi wa Njombe kutumia njia nyingine kujikinga na baridi badala ya kuota moto kama ambavyo wengi wamekuwa wakifanya, kwa kuwa kufanya hivyo ni hatari kwa maisha yao.

"Wewe unaona chumba chako ni kidogo na unatumia mkaa ndani, hiyo ni hatari nyingine na huko lilikotokea tukio chumba ni kidogo na kina dirisha moja na dogo sana." Alisema na kuongeza: "Acheni kulala na jiko ndani ya nyumba, sasa hivi ni hatari, tafuteni nguo nzito nzito za kuzuia baridi, lakini sio moto wa mkaa."

Kamanda Issah alisema tukio hilo ni la tatu kutokea mkoani Njombe, na kulitaja tukio jingine la kumkuta mkazi wa Songea aliyekuwa mhudumu wa baa moja mjini Njombe kufariki ndani ya nyumba kukiwa na jiko la mkaa na mwingine akifariki wilayani Wanging'ombe katika chumba ambacho kilikuwa na jiko la mkaa.

Mmiliki wa nyumba hiyo, Amani Samsoni Mwalongo, ambaye alikuwa mtu wa kwanza kushuhudia tukio hilo," alisema:

"Nilifuatilia kwa majirani wanasema yule mwanamke alikuwa anaelekea Madaba, akakosa nauli na huyu kijana kwa kuwa yupo pale kwenye magari akamwambia njoo upumzike kwanza na kesho nitakusaidia nauli ya kukufikisha kwenu. Kwa hiyo hili ni tukio linalohuzunisha sana.



Abiria wakiwa kwenye daladala linalofanya safari zake kati ya eneo la Kivule na Banana, jijini Dar es Salaam, huku wakiwa hawajachukua tahadhari yoyote ya kujikinga na maambukizi ya COVID-19, licha ya serikali kutangaza uwepo wa mlipuko wa tatu wa ugonjwa huo hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Majaliwa aiongeza siku kamati moto Kariakoo

**Na Christina** Mwakangale

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, ameiongezea muda wa siku saba kamati iliyoundwa kuchunguza chanzo cha moto kwenye Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Amesema uamuzi huo ni baada ya kamati hiyo inayoongozwa na Mkoa wa Dar es Salaam, kumwomba kuongezewa siku zaidi ili kufanya uchunguzi wa kina hususani katika uhandisi wa jengo la soko hilo.

Majaliwa alitangaza uamuzi huo jana katika Baraza la Eid El Hajj lililofanyika katika Msikiti wa Mtoro, Ilala jijini, akiongezea muda kamati hiyo hadi Julai 25, mwaka huu, kutoa taaifa yake.

"Miundombinu ya umeme pale haipo salama, jengo limepigwa moto lote, huwezi kujua usalama na kamati ya usalama imefanya kazi yake vizuri.

"Kamati niliipa siku saba. Nikiwa Morocco waliniomba ridhaa niwaongezee muda ili waingie hasa katika uhandisi wa kulipima jengo zima kwamba 'moto uliowaka siku mbili umeshaiunguza saruji?

Alisema hivi sasa hazitarusiwa biashara kwa mtu yeyote kwenye eneo hilo, lakini watakaohitajika kutoa ushahidi, watoe ushirikiano.

Baada ya tukio la moto huo lilotokea Julai 11, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza kwa kina kujua chanzo cha moto huo, huku Waziri Mkuu akiunda Kamati ya Mkoa na kuipa siku saba kutoa taarifa ya uchunguzi wa chanzo cha moto huo.

DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA UNUNUZI WA **VIFAA VYA UJENZI, VIFAA VYA NYUMBANI, VIFAA VYA KUANDIKIA.**

HIVYO SHIRIKA LA DANISHI LIMERUDIA KUTANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USIFUTE KWENYE BEI
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENYE MFUMO WORD/EXCEL.
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA VILE KIAMBATISHO A.1, KIAMBATISHO A.2, CHETI CHA KUKUBALI TUZO YA ZABUNI NA KANDARASI, WASIFU WA MUUZAJI NA FOMU YA USAJILI, HALI YA MKATABA WA JUMLA WA DRC, MAELEZO YA KAMPUNI, KANUNI YA MWENENDO WA WASAMBAZAJI WA DRC BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE KAMILI, SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

**NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 22.07.2021 HADI TAREHE 4.08.2021 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.**

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 06237423991 au BARUA PEPE jean.kabore@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 6.08.2021 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI PEKEE KUTOKANA NA MLIPUKO WA UGONJWA WA CORONA.**

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

216368301

# Samaki waliokufa wazagaa ufukweni

**Na Romana Mallya**

SAMAKI waliokufa wameonekana kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Mamlaka za serikali zimekiri kuonekana kwa samaki hao na tayari uchunguzi umeanza kubaini chanzo chake.

Mmoja wa mashuhuda aliyekuwa sehemu ya timu ya maofisa wa serikali waliozuru eneo la tukio jana, aliliambia Nipashe kuwa suala hilo lipo kwenye uchunguzi wa Jeshi la Polisi na mamlaka zingine za serikali na tayari sampuli zimechukuliwa kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Ofisa huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa si msemaji, alisema samaki hao walionekana kwenye eneo hilo Aga Khan.

"Tulijaribu kukusanya na zilifika kilo zaidi ya 150, ila kwa sasa ni mapema kulizungumzia suala hili," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alipoulizwa kuhusiana na samaki hao, alisema kwa wakati huo hakuwa na taarifa na kuahidi kutuma wataalamu wake kwenda eneo la tukio.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dk. Ismail Kimirei, alikiri samaki hao walionekana eneo hilo la ufukwe lakini polisi waliingia kati mwanzoni na waliwapa taarifa maofisa wa Wizara ya Mifugo ambao mara moja walikwenda eneo la tukio.

"Tukafika na watu wa wizara tumechukua sampuli na zingine zimekwenda maabara ya taifa ya wizara na polisi kwa ajili ya kupeleka kwa Mkemia Mkuu, tunasubiri majibu.

"Samaki waliokusanywa walikuwa ni wa aina mbalimbali lakini wengi wao ni watoto na ziliokotwa kilo 160," alisema. Hata hivyo, alisema matukio kama hayo ya samaki kukutwa ufukweni wakiwa wamekufa wakati mwingine hutokea wanapokosa hewa ya Oksijeni baharini.

Alisema mpaka sasa hawajapata taarifa za kuwapo kwa samaki wakiwa wamekufa sehemu nyingine zaidi ya ufukwe uliopo karibu na Hospitali ya Aga Khan.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kushoto), akiteta jambo na Mbunge wa Jimbo la Mchinga, Salma Kikwete, wakati wa mkutano wa kusikiliza kero za wananchi uliofanyika Kata ya Milola katika Manispaa ya Lindi, jana. **PICHA: HAPPY SHAYO**

# Wanaodai fidia Bandari Bagamoyo watulizwa

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema wananchi wanaodai fidia katika eneo la bandari na la viwanda la EPZA wilayani Bagamoyo, wanatakiwa kuwa watulivu wakati utaratibu unaendelea kufanyika ili waweze kupata stahiki zao.

Lukuvi aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kuzungumza na wananchi kutatua migogoro ya ardhi kwenye kampeni ya kutokomeza migogoro ya ardhi iliyoanzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge.

Alisema wataalamu wanaendelea kuhakiki eneo ambalo limechukuliwa na serikali, wapo waliolipwa fidia na wengine watalipwa baada ya uhakiki.

"Wale ambao wameshalipwa fidia waondolewe na wale ambao bado wasubiri asiongezeke mtu akaanzisha ujenzi upya atabomolewa, tunasubiri timu ilete majibu na tutafuata taratibu," alisema.

Aidha, waziri huyo aliagiza halmashauri kuwalipa fidia wananchi zaidi ya 1,000 ambao viwanja vyao vimechukuliwa na serikali.

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Mkoa kuhakikisha kila wilaya inakuwa na daftari la taarifa za migogoro ya ardhi, ili iundwe timu ya kuratibu na kushughulikia migogoro hiyo.

Ameitaja Wilaya ya Bagamoyo eneo la Mapinga kuongoza kwa migogoro ya ardhi, ambayo imechangiwa na viongozi wa ngazi za chini wakiwamo mabalozi.

Alisema migogoro hiyo imekuwa kero na kuwafanya wananchi kukosa amani na kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

Alisema ana majina ya watu 54 wanaodaiwa kuwa vinara wa kuuza ardhi katika Wilaya ya Bagamoyo, wakiwamo viongozi wa mitaa.

Lukuvi aliwataka wakazi wa Bagamoyo kuacha kuvamia maeneo ya serikali, ambayo hayajaendelezwa, likiwamo la Lazaba linalomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema viongozi wa serikali wanatakiwa kulinda maeneo hayo pamoja na la Lazaba yanayomilikiwa na serikali, kwani ipo mipango ya uwekezaji, hivyo yeyote atakayevamia asitarajie kulipwa fidia.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliahidi kufanyia kazi maelekezo ya waziri kukomesha uvamizi wa mkoa huo, na kwamba migogoro mingi wilayani humo inadaiwa kuchangiwa na watendaji na viongozi wa kisiasa.

Kwa mujibu wa Ofisa Ardhi Wilaya ya Bagamoyo, Wendeline Izina, awamu ya kwanza wananchi 2,258 walitambuliwa kati yao 1,155 wamelipwa fidia katika eneo la EPZA lenye ukubwa wa hekta 9,800.

Izina alisema katika eneo la bandari lenye ukubwa wa hekta 887, wananchi na taasisi 2,211 walitambuliwa na kwamba 2,181 wameshalipwa fidia.

# Mama wa aliyeuawa kwa risasi baa anena

**Na Mwandishi Wetu**

MAMA mdogo wa marehemu Gift Mushi, aliyeuawa kwa risasi sita na Alex Kosoro (37) maarufu kama 'Simba', wakati wakiwa baa ya Lemax, Sinza Kwa Remmy, Dar es Salaam, amefunguka na kumwelezea mwanawe kama tegemeo pekee na waliongea kwa simu siku mbili kabla ya kuuawa.

Alisema amemlea Gifti tangu akiwa na miaka tisa baada ya mama yake mzazi kufariki, na kwamba alikuwa na mchango mkubwa kwenye familia kwa kuwa alikuwa mfariji mkuu wa maisha na kumsaidia kama mama yake.

"Kabla sijapata hizi taarifa niliondoka nyumbani (Kijichi) kwenda kwenye biashara zangu maeneo ya Tabata, lakini sikuweza kufika niliishia TAZARA baada ya mwili kukataa nikarudi nikafikia kwa jirani yangu nikamwambia najisikia vibaya, akaniambia nenda kapumzike."

Alisema baada ya kuingia ndani alipigiwa simu na mtoto wa kaka yake (Mama Gifti) kuwa mwanawe amepigwa risasi "Nilimuuliza ni Gifti au nani, akaniambia ni Gifti, sikuweza kujibu lolote, nilikaa kimya kwanza sikuweza kumuhoji chochote, baada ya dakika tano nikapigiwa tena simu mama, Gifti kapigwa risasi, nikauliza tatizo ni nini wakasema hawajajua."

"Ni mengi namkumbuka mtoto wangu hasa upendo wake, alikuwa anawasaidia wadogo zake, mara ya mwisho kuwasiliana naye siku mbili kabla ya kupigwa risasi nilichart naye akanipigia kupitia namba ya rafiki yake, tuliongea mengi kuhusu maisha nikawa namsihi aendelee kupambana maana maisha ni magumu," alisema.

Naye, mdogo wake Gift, Yusuph, alisema alirudi nyumbani na kumkuta mama yake analia akamwambia ajiandae waende hospitali kwa kuwa kaka yake amepigwa risasi na ana hali mbaya.

"Niliingia kuoga natoka naambiwa kaka Gifti ameshapoteza uhai, tuliwasiliana muda mfupi tulikuwa na mipango yetu ya maisha. Gifti alikuwa na mchango mkubwa kwa kuwa alimpa moyo anaposhindwa, anapojihisi mnyonge kwamba maisha lazima kupambana tutoboe."

Wakati huo huo, Mwili wa Alex aliyetenda mauaji hayo umeagwa katika Kanisa Katoliki Parokia ya Muhimbili, na baadhi ya wasanii wa Bongo Movie walishiriki kumuaga.

Katika tukio hilo, Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, walisema hakuna kesi kwa kuwa aliyeua naye alijiua.

# Kimya chatawala timu ya uchunguzi stendi Mwenge

**Na Mwandishi Wetu**

KIMYA kimetawala kwa taarifa ya timu ya uchunguzi wa mradi wa kituo kipya cha daladala Mwenge, iliyopewa wiki mbili kuanzia Juni 20, mwaka huu, kukamilisha kazi hiyo na kuikabidhi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.

Timu hiyo ilipaswa kukamilisha kazi yake Julai 4, mwaka huu, lakini sasa ni wiki ya tano, na hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na ujenzi umesimama kwa muda mrefu.

Nipashe ilimtafuta Waziri Ummy akiwa mjini Bagamoyo Julai 18, mwaka huu, alijibu kuwa anakwenda Dodoma Juni 19 (Jumatatu iliyopita) atapata mrejesho wa kamati na atatoa majibu ya maswali atakapofika jijini humo.

Aidha, hadi sasa hakuna taarifa yoyote iliyotolewa kuhusu kusuasua kwa ujenzi huo.

Juni 20, mwaka huu, Waziri Ummy alitembelea ujenzi huo na kueleza kutoridhishwa na kusuasua kwa ujenzi huo, na kwamba amekuwa akipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

"Huu mradi ulipaswa kukamilika Mei 2, mwaka huu, lakini hadi sasa ni Juni na ujenzi wake umefikia asilimia 46, nasimamisha ujenzi wake kuanzia sasa na kuunda timu ya kuchunguza," alisema Waziri Ummy.

Hivyo, Waziri Ummy alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuunda timu hiyo haraka na kueleza kuwa itafanya kazi katika kipindi cha wiki mbili, itachunguza pia miradi miwili ambayo ni Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Manispaa ya Kinondoni, Ujenzi wa Jengo la Utawala la Manispaa ya Kinondoni.

Mbali na hilo, Waziri Ummy pia alitangaza kumsimamisha kazi Mhandisi wa Manispaa ya Kinondoni, Isaak Mpaki, kutokana na kushindwa kuishauri vizuri Manispaa ya Kinondoni juu ya ujenzi wa miradi hiyo mitatu.

"Kuna figisu kwenye hii miradi, miradi haikamiliki, kila mtu anasema la kwake, huu mradi (Stendi ya Mabasi) ungekamilika ungeingiza faida ya Sh. milioni 480 kwa mwaka, tungejenga shule, hospitali, lakini hadi sasa hakuna kitu," alisema Waziri Ummy.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Spora Liana, alisema gharama ya ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 4.898, kwamba mkandarasi (361 JWT Lugalo) alikabidhiwa mradi Julai 27, mwaka jana.

Alisema ilipofika Mei 2, mwaka huu, ujenzi wa mradi huo ulifikia asilimia 46, hadi sasa Sh. bilioni 1.558 zimeshatumika.

"Changamoto kubwa ni vifaa kutoagizwa kwa wakati, vibarua wachache ambapo mkandarasi badala ya kutumia askari anaajiri raia, pamoja na kuchelewa kulipwa mishahara yao na kuja ofisi kwangu kunilalamikia," alisema Liana.

Mkandarasi wa mradi huo, Luteni Kanali David Luoga, alisema Aprili mwaka jana walianza kazi ya ujenzi wa stendi hiyo, kazi yao ni kujenga lakini vifaa vya ujenzi vinaletwa na Manispaa ya Kinondoni.

"Ilipofika Julai mwaka jana mtiririko wa vifaa haukuwa mzuri, vikawa vinakuja kwa kusuasua, ilipofika Septemba tuliandika barua ya kuomba vifaa vyote vinavyohitajika kufika eneo la mradi lakini hadi sasa havijafika," alisema Luteni Kanali Luoga.

Alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo ni kutokuwapo kwa utekelezaji wa maamuzi yaliyoingiwa, viongozi wa Manispaa ya Kinondoni kutokuwa na maamuzi.

## Samia atoa bil. 1.5/- matengenezo barabara za ndani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. bilioni 1.5 kwenye Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kwa ajili ya kutengeneza barabara za ndani za kiwango cha changarawe ili kufungua uchumi.

Akizungumza na wakazi wa jimbo hilo wakati wa ugawaji wa kitoweo cha nyama ya kusherekea Siku kuu ya Eid, Mbunge wa jimbo hilo, Hamis Shomari (Babu Tare), alisema fedha hizo zimetolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Barabara Vijijini na Mijini (TARURA). Alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha hizo kwa kipindi kifupi ambacho kitatumika kutengeneza barabara zilizopo katika kata ambazo wakulima wanazalisha mazao mbalimbali ili kuwasaidia kurahisisha shughuli za usafiri wa mazao yao.

Alisema Jimbo hilo la Morogoro Kusini ndiyo linaongoza kwa kuzalisha mazao mbalimbali yakiwamo matunda ya aina zote yanaliwa katika mikoa mbalimbali, mboga pamoja na mazao ya nafaka kama mahindi na mpunga.

## Serikali yafuta uagizaji mbolea kwa zabuni

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imefuta utaratibu wa kuagiza mbolea kwa zabuni, baada ya kubaini haiwasaidii wakulima.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kwamba kwa sasa wigo wa uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi umefunguliwa kwa wafanyabiashara wenye nia ya kufanya biashara hiyo.

"Tunaamini hatua hii itasaidia mbolea kuingia kwa wingi nchini hivyo wafanyabiashara watakuwa na bei ya ushindani, haimuumizi mkulima, pia tunachoangalia sisi mbolea inayoletwa iwe na viwango vya ubora unaotakiwa," alisema.

Alisema mfumo wa zabuni haujawasaidia kwa kuwa kampuni nyingi zinazojitokeza lakini yanachukuliwa machache, bei inapangwa ambayo siyo rafiki kwa wakulima.

"Japo hatuna uwezo wa kushusha bei kwenye soko la dunia lakini tunahitaji kuona wafanyabiashara wanasaidia kuwezesha mbolea kupatikana kwa wingi, Serikali inafanya juhudi ikiwamo kupunguza gharama za kulipia maghala ya kuhifadhi,"alisema Prof. Mkenda.

Alibainisha lengo la serikali ni kuwaona wakulima wanapata faida kutokana na kilimo, ndiyo maana haijaweka kodi yoyote kwenye mbolea.

Mkurugenzi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Dk. Anselm Moshi, alisema ununuzi wa mahindi ni kati ya Sh.250 hadi 480 ikitofautiana kwenye mikoa husika.


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2021 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2021 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 831.27 | 567.14 |
| 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 4,832.27 | 4,610.48 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 33,550.32 | 35,629.77 |
| 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 985.74 | 189.57 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 115.78 | 32.86 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,374.21 | 30,529.38 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 48,480.24 | 44,355.70 |
| 12 Mali Nyingine | 1,172.60 | 1,164.51 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 927.19 | 1,027.82 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **127,269.62** | **118,107.24** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 37,655.00 | 29,725.00 |
| 18 Amana za Wateja | 48,469.08 | 47,662.11 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,789.84 | 1,828.45 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 594.11 | 668.33 |
| 28 Madeni | - | - |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **88,508.02** | **79,883.89** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **38,761.60** | **38,223.35** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 283.58 | 0.00 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 4,511.99 | 4,795.57 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,136.03 | 597.78 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,761.60** | **38,223.35** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 9,890.17 | 7,779.63 |
| 39 Mikopo Chechefu | 1,403.76 | 1,394.56 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 502.62 | 456.48 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 30.46% | 32.36% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.87% | 3.11% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 56.85% | 57.88% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.09% | 37.56% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 93.81% | 93.73% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 11.29% | -4.75% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 7.76% | -2.85% |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2021 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Juni 2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,372.61 | 2,076.28 | 4,717.04 | 4,204.70 |
| 2 Gharama za Riba | 809.28 | 789.45 | 1,620.45 | 1,571.07 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,563.32** | **1,286.83** | **3,096.60** | **2,633.63** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 46.14 | (171.55) | 138.47 | (52.18) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **174.29** | **147.48** | **345.61** | **339.50** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 17.52 | 60.31 | 65.35 | 96.24 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 156.77 | 87.16 | 280.26 | 243.26 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **883.22** | **984.85** | **1,627.70** | **1,672.69** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 364.75 | 325.61 | 699.36 | 645.76 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 6.69 | 4.57 | 11.86 | 9.35 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 511.79 | 654.67 | 916.48 | 1,017.58 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **808.25** | **621.00** | **1,676.03** | **1,352.62** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 270.00 | 150.00 | 540.00 | 360.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **538.25** | **471.00** | **1,136.03** | **992.62** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 16 | 14 | 35 | 30 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 16 | 14 | 35 | 30 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.81% | 1.75% | 1.88% | 1.84% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.66% | 5.13% | 5.93% | 5.44% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 50.83% | 68.66% | 47.29% | 56.26% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.63% | 5.40% | 5.46% | 5.51% |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2021 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 538.25 | 597.78 | 1,136.03 | 992.62 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 100.63 | 100.56 | 201.19 | 219.06 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | (4,124.54) | 4,069.15 | (55.39) | (634.15) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 8,736.97 | (3,861.80) | 4,875.18 | 1,152.34 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 281.25 | 73.57 | 354.82 | 333.55 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (2,956.99) | 1,950.84 | (1,006.14) | (1,470.35) |
| Kodi iliyolipwa | (270.00) | (270.00) | (540.00) | (360.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2,305.56** | **2,660.12** | **4,965.68** | **233.07** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (0.00) | (5.35) | (5.35) | (13.12) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (3,218.91) | 557.44 | (2,661.47) | (9,399.98) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(3,218.91)** | **552.10** | **(2,666.81)** | **(9,413.10)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (123.94) | - | (123.94) | (131.40) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(123.94)** | **-** | **(123.94)** | **(131.40)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,037.28) | 3,212.21 | 2,174.93 | (9,311.43) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 40,109.04 | 36,896.83 | 36,896.83 | 48,369.87 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **39,071.76** | **40,109.04** | **39,071.76** | **39,058.44** |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/06/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,136.03 | - | - | - | **1,136.03** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (242.23) | 242.23 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **5,648.01** | **283.58** | **-** | **-** | **38,761.59** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,658.29 | - | - | - | **1,658.29** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 787.23 | (787.23) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |

**BAADHI YA MAELEZO
KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 Juni 2021**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 19-07-2021 |

**Canara Bank (T) Ltd
Head Office Dar Es Salaam Branch
Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania
E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532
www.canarabank.co.tz**

216368102

# MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

## *Tunasubiri utekelezaji agizo la Simbachawene*

**JANA** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alipiga marufuku kuingia na silaha kwenye maeneo ya starehe kama baa, kumbi za muziki, harusi na mengine kwenye mikusanyiko ya watu.

Aidha, alisema ni lazima kuwapo utaratibu wa wahusika na maeneo hayo kufanya ukaguzi mlangoni kabla ya watu kuingia ndani.

Agizo la Waziri huyo limekuja siku chache, baada ya kutokea tukio la Alex Koroso (37), kummiminia risasi sita Gifti Mushi, na kumuua kisha naye alijiua kwa kujipiga risasi wakiwa kwenye baa ya Lemax, Sinza Dar es Salaam.

Baada ya tukio hilo kulikuwa na mjadala mkali kwenye mitandao ya kijamii, juu ya namna wanaomiliki silaha wako huru kwenda nazo kila mahali na hakuna utaratibu wa kukagua na hata kama ukaguzi unafaponyika, siyo wa kuhakikisha usalama.

Mathalani, tukio la Alex alianza kufanya vurugu tangu asubuhi kwa kuwa alifika kwenye baa hiyo akiwa ametoka kukesha kwenye baa nyingine, aliendelea kunywa na kuna wakati alimwaga risasi mezani na moja kuanguka chini ikaokotwa na msimamizi wa baa hiyo lakini aliendelea na starehe zake.

Tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu na, ni jambo jema, lakini tunapenda kutahadharisha kuwa isiwe ni zimamoto kwa kuwa kuna tukio limetolea bali iwe ni utaratibu endelevu na ufuatiliwe.

Lakini bado kuna maswali mengi kwa kuwa zipo baa ambazo ni za wazi hazina mlango mmoja maalum wa kuingilia, bali unaweza kuingia kokote na kukaa ukahudumiwa, je, hili nalo litafanyikaje katika kudhibiti?

Pia, kuna baa zinazoanzishwa kwenye maduka ya vinjwaji kwa kuweka viti kadhaa nje kwa ajili ya watu kupata kinywaji, nako hakuna uratatibu wa kukagua.

Hakuna ubishi kwamba ukaguzi haufanyiki kuanzia kwenye kumbi za sherehe na baa, kwa kuwa watu hujiingilia tu, lakini yapo maeneo ambayo ukaguzi haufanyiki ipasavyo bali walinzi wanaruhusu watu kupita kuendelea na shughuli zao, na hili lipo katika moja ya eneo maarufu la manunuzi na matembezi (jina linahifadhiwa).

Waziri kutoa agizo ni jambo moja, utekelezaji ni jingine, ni muhimu ukatolewa utaratibu wa namna ya kufunga vifaa maalum vya ukaguzi na kufuatilia utekelezaji mara kwa mara, kwa kuwa inawezekana kufanyika kwa muda mfupi baada ya hali kutulia maisha yakaendelea.

Kama vifaa hivi vitafungwa, ni muhimu kufuatilia usalama wake, lakini kutoa elimu kwa wamiliki kuwa wanapoona hali ya kutoweka kwa amani wasiangalie uwezo wa mteja au fedha atakazolipa, bali usalama wa waliopo kwenye eneo hilo.

Tukio la Alex limeacha funzo kwa wamiliki na wasimamizi wa baa kuwa wanapaswa kuhakikisha usalama wa wateja wao, kwamba kama mtu anaonyesha lolote la kuvunja amani, hatua zichukuliwe mapema.

Pamoja na uamuzi huo, ni muhimu kupima afya ya akili ya watu wanaomiliki silaha hizo, kwa kuwa yaliyokuwa yanaendelea kwenye baa hiyo yalionyesha siyo kwamba mtendaji alikuwa amelewa tu, bali kulikuwa na tatizo jingine kubwa.


Ni muhimu kupitia kila mara umiliki wa silaha kama wahusika wanafuata taratibu, kwa kuwa baada ya tukio hili imetokea mifano mingi inayoeleza kuwa wapo watu hutumia kutishia watu au kuonyesha kuwa wanazimiliki, jambo ambalo halitakiwi kuwa huko.

Agizo la waziri lina nia njema kabisa, ila bado tunasisitizo kuwe na utekelezaji isije ikawa ni zimamoto kwa kuwa kuna tukio limetokea na kusababisha majadala kwenye mitandao ya kijamii.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## *Itapendeza kila Mkuu wa Wilaya, Mkoa wadhibiti wasiovaa barakoa*

**KATIKA** jitihada za kukabiliana na ugonjwa wa corona, serikali imeshaagiza wananchi kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa sehemu zenye mikusanyiko, ili kujikinga na wimbi la tatu lililoibuka katika mataifa mbalimbali.

Wakuu wa mikoa na wilaya nao wameshapewa maelekezo ya kuhakikisha wanatimiza agizo hilo kwa kuzishirikisha kamati za afya ya msingi, namna wanavyotekeleza, nayo inaingia katika tafsiri na thamani fulani ya utumishi, kuwa kipimo cha utendaji wao kikazi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anaagiza wananchi kuchukua tahadhari kwa kurejesha utaratibu wa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na matumizi ya vitakasa mikono.

Kwa mujibu wa waziri huyo, hatua hizo zinachukuliwa kwa kuwa Tanzania inazungukwa na nchi nyingi za Afrika Mashariki, majirani wa pembe za Afrika na safari zaidi, wageni wanapokewa kila kukicha kutoka pembe mbalimbali duniani.

Dk. Gwajima anabainisha kuwa, utaratibu wa kuvaa barakoa unapuuzwa, hali ambayo ni hatari kwa kuwa Tanzania imezungukwa na nchi ambazo tayari zinapigwa na wimbi la tatu la corona.

Kwa kuwa serikali imeshatoa miongozo, kilichobaki ni utekelezaji, wananchi wachukue tahadhari, pia suala la kutoa elimu lingechukuliwa kwa uzito kuanzia ngazi ya chini ili kudhibiti ugonjwa huo.

Elimu inapaswa kuanzia ngazi ya familia na kupanda juu hadi kwenye wilaya, mikoa na hata taifa kwa ujumla, ili kuondoa uzembe uliopo wa baadhi ya watu kutovaa barakoa kwenye mikusanyiko.

Si vibaya suala la kuvaa barakoa likihimizwa nchi nzima na kusimamiwa kikamilifu badala ya kusimamiwa na baadhi ya viongozi wa mikoa na wilaya huku maeneo mengine kukiwa kimya.

Wapo baadhi ya wakuu wa mkoa na wilaya, ambao kwenye maeneo yao wamepiga marufuku abiria kusafiri katika mabasi bila ya kuvaa barakoa, wakiwataka wananchi wao wawe salama.

Mfano hai ni kwamba, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameshapiga marufuku abiria katika mkoa huo kusafiri bila kuvaa barakoa, lengo ni kuhakikisha maambukizi ya corona yanadhibitiwa.

Wakati Mtaka akipiga marufuku, Mkuu wa Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Said Mtanda, anazitaka mamlaka za usafirishaji kuzuia mabasi kutoka stendi kama kutakuwa na abiria asiyevaa barakoa ili za kujikinga na corona.

Iwapo marufuku hiyo itapigwa nchi nzima, dhahiri kila Mtanzania atakuwa katika hatua ya kuona umuhimu wa nyenzo barakoa kujinga na kuwakinga wengine, badala ya kusikia kwenye wilaya moja na mkoa viongozi wake wakivalia njuga barakoa.

Wananchi wa wilaya hizo na mikoa hiyo wanaweza kuchukua hatua, lakini zikaharibiwa na wale ambao kwenye maeneo yao hajazuiwa kusafiri bila kuchukua tahadhari, ikiwamo kuvaa barakoa.

Itapendeza zaidi kuona, iwapo hatua kama hizo zitachukuliwa na viongozi wa wilaya na mikoa yote, ili kuwasaidia wananchi wao kujikinga dhidi ya wimbi la tatu la corona ambalo serikali imekiri athari zake tayari ziko nchini.

Watu wamekuwa wakisongamana bila kuvaa barakoa, hivyo ni vyema wakaagiza wizara husika kukachukua hatua kwa uzito, ikiwa ni pamoja na viongozi kwenye maeneo yao kuelekeza wananchi kuchukua tahadhari.

Viongozi wote wanapaswaa kuchukua hatua kama zilivyochukuliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Mkuu wa Wilaya ya Moshi. Watanzania kila mmoja kwa nafasi yake na anapaswa kuchukua hatua zinazoelekezwa na mamlaka zilizopo.

Si rahisi wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania kufika kila sehemu, bali maagizo ambayo inatoa kwa viongozi wa wilaya na mkoa, yanatosha kupewa uzito, ili kuhakikisha ugonjwa huo haupati nafasi.

Ikumbukwe kuwa, tangu ugonjwa huo kuingia nchini, kumekuwapo na elimu mbalimbali zikiwamo zinazotolewa 'vijiweni' ambazo ni kinyume na maelekezo ya wizara husika kuhusu kujikinga na ugonjwa wa UVIKO.

## Simbachawene akishtukia kituo cha polisi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameahidi kuzungumza na IGP Simon Sirro, kukifunga Kituo cha Polisi cha Mtitu, wilayani Kilolo kinacholalamikiwa kwa madai ya kujengwa kwa maslahi ya watu binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani hapa baada ya kuhitimisha ziara ya siku mbili, Waziri Simbachawene, alisema, amekutana na mambo mbalimbali likiwamo ombi la Mbunge wa Kilolo, Justin Nyamoga, kuomba kujengwa kwa kituo cha polisi cha Wilaya ya Kilolo jirani na makao makuu ya wilaya hiyo na uchakavu wa Kituo cha Polisi Mtitu.

Alisema alifanya ziara katika kituo cha Mtitu na kukuta askari wanaoshinda kituoni bila kazi na kwamba hakina tija kutokana na eneo hilo kuwa na wananchi wachache.

Pia alisema umbali wa kituo cha Kilolo na Mtitu ni kilomita tano pekee.

Aliahidi kushauriana na IGP ili kuangalia uwezekano wa kukifunga na askari wanne waliopo wapelekwe maeneo mengine ambayo yana uhitaji wa askari.

Pia, alisema suala la ulipaji wa fidia ya zaidi ya Sh. milioni 100 katika eneo la Kilolo ambako yatajengwa makao makuu ya polisi, litafanyiwa kazi ili kuwapo kwa makao makuu ya polisi jirani ya makao makuu ya wilaya tofauti na sasa kutumia majengo ya TAZAMA eneo la Tarafa ya Mazombe kama makao makuu ya polisi wilaya.

Katika hatua nyingine, alisema ziara yake imemaliza mgogoro wa ardhi kati ya Magereza Mufindi na raia ambao walikuwa wakigombea eneo lenye ukubwa wa hatua tano na kusababisha suala hilo kufika kwa Waziri Mkuu na uamuzi wake ni Magereza kuachia kipande hicho cha ardhi kwa familia iliyokuwa ikilalamikia eneo hilo.

Pia, Waziri Simbachawene ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama mkoani Iringa kushirikiana kufichua raia wa kigeni wanaofanya kazi kinyemela kwenye kampuni mbalimbali.

Alisema wapo baadhi ya raia wa kigeni kutoka China ambao walikuja kwa kibali cha miezi mitatu kama wataalamu, lakini muda wao umekwisha na bado wanaendelea kufanya kazi nchini jambo ambalo alilosema ni hatari.

Alitaka vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana kuwafichua raia hao kwa kuwa kuendelea kufanya kazi katika kampuni na taasisi binafsi bila kuwa na vibali ni kosa.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kupambana na uhalifu ikiwa ni pamoja na kukomesha matukio hayo.

Alisema kuwa suala la uhalifu halikubaliki na hatutakubali kuona wananchi wakinyanyasika na vitendo vyovyote vya uhalifu.

# Polisi wateketeza mashamba ya bangi

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi Wilaya ya Lindi, linawashikilia watu watano, kwa madai ya kujihusisha na kilimo cha bangi.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alibainisha hayo alipokuwa anazungumza na Nipashe wakati wa uteketezaji wa zao hilo lililofanyika eneo la msitu wa Mangalanganda.

Amewataja wanaoshikiliwa ni Salum Mtopwa (70), Saidi Mohamedi Songea (43), Somoe Mohamedi (31), Seif Issa (20) na Mudhihili Omari (20), wanaodaiwa kumiliki mashamba manne ya bangi yanayoelezwa kuwa na ukubwa wa ekari saba.

Kitinkwi akizungumza tukio hilo wakati polisi wakishirikiana na wananchi wa Kijiji cha Namkongo, alisema mtuhumiwa Mtopwa licha ya kujihusisha na kilimo hicho pia anamiliki bunduki aina ya Rifle.

Amesema mtuhumiwa huyo huenda silaha hiyo anaitumia kinyume na maombi yaliyomwezesha kumilikishwa kwani amebainika kujitengenezea risasi badala ya kununua katika maeneo yaliyoidhinishwa kisheria.

"Bunduki hii tunaifanyia uchunguzi iwapo anaimiliki kisheria au laa," alisema Kamanda Kitinkwi.

Pia, alisema wakati wa uteketezaji wa mashamba hayo, askari wakishirikiana na wananchi walikamata viroba kadhaa vya bangi iliyokwishakauka na mbegu zake vilivyofichwa maeneo mbalimbali ya pori.

Kamanda Kitinkwi amesema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa uchunguzi.



Wanachi wa Kijiji cha Namkongo, Kata ya Mipingo, Tarafa ya Mchinga, wakisaidiana na askari wa Jeshi la Polisi, katika zoezi la uteketezaji wa zao la bangi zilizopandwa eneo la Msitu wa Mangalanganda, wilayani Lindi, mkoani Mtwara jana, ambapo watu watano wamekamatwa. **PICHA: SAID HAMDANI**

## Mpango kushiriki misa kumkumbuka Mkapa

**Na Abadallah Khamis,** MTWARA

MAKAMU wa Rais, Dk. Isdori Mpango, anatarajiwa kuwaongoza Watanzania katika misa ya kumbukumbu ya kutimiza mwaka mmoja tangu kufariki kwa Rais wa Awamu ya Tatu, hayati Benjamini Mkapa.

Misa hiyo itafanyika katika Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi na pia Dk. Mpango anatarajiwa kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo na kuzungumza na wakazi wa mkoa wa Mtwara, katika ziara ya siku tano. Akizungumza na waandishi wa habari, jana Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali, Marco Gaguti, alisema Dk. Mpango atawasili mkoani humo kesho na Julai 24 atakuwa wilayani Masasi kwenye kijiji cha Lupaso kwa ajili ya kuhudhuria misa ya kumkumbuka hayati Mkapa.

"Siku hiyo hiyo baada ya misa Makamu wa Rais atazindua soko katika Wilaya ya Masasi na siku inayofuata atazindua kiwanda cha kubangulia korosho katika Wilaya ya Newala, kiwanda hiki kina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 800," alisema Brigedia Jenerali Marco Gaguti.

Alisema pia, Julai 26 ataweka jiwe la msingi katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini na Julai 27, atamaliza ziara yake mkoani humo.

# Wanafunzi HKMU walilia mikopo

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wengi wa udaktari katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), wamelalamikia kukosa mikopo ya bodi licha ya kuwa na sifa.

Hayo yalisemwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho, Meshack Morice, mbele ya Mkuu wa Chuo hicho, Anne Makinda, aliyetembelea chuo hicho mwanzoni mwa wiki hii.

Alisema pamoja na serikali ya wanafunzi kujitahidi kusaidia taarifa sahihi za wanafunzi zinawasilishwa kwa Bodi ya Mikopo, lakini kumekuwa na mwitikio hafifu na wanaopata ni wachache.

Morice alisema hali hiyo imesababisha changamoto kubwa kwenye ulipaji wa ada kwa wanafunzi wengi pamoja na gharama za malazi na chakula hali ambayo alisema inawaathiri wanafunzi hao kitaaluma.

Alitoa takwimu zinazoonyesha asilimia ndogo ya wanafunzi wanaopata mikopo chuoni hapo akisema wanufaika wamepungua kwa zaidi ya asilimia 100 chuoni hapo ingawa wana kada zinazohitajika zaidi nchini.

Alisema kati ya wanafunzi 276 wa mwaka wa kwanza ni 29 pekee wanaopata mikopo ambayo ni sawa na asilimia 10.5, wanufaika wa mwaka wa pili ni 22 kati ya 211 ambayo ni sawa na asilimia 10.4 huku mwaka wa tatu wanufaika wakiwa 46 kati ya 195 ambayo ni sawa na asilimia 23.

Morice alisema wanufaika wa mwaka wanne ni 56 kati ya wanafunzi 240 ambayo ni sawa na asilimia 23, mwaka wa tano wanufaika wa mikopo ni 77 kati ya wanafunzi 181 ambayo ni sawa na asilimia 42.5 huku mwaka wa tano waliomaliza wakiwa 173 kati ya 187 ambayo ni sawa na asilimia 92.5.

Pia, alisema serikali ya wanafunzi imefanyakazi kubwa kushirikiana na chuo na kwa kufanya hivyo wamepata mafanikio makubwa kitaaluma na katika nyanja mbalimbali.

Alisema wanafunzi wamefanikiwa kufanya semina za kitaaluma kwa kushirikiana na idara zote za kitaaluma za chuo hicho na hiyo imesaidia kuwaongezea ujuzi wa mambo mbalimbali kwa wanafunzi wa miaka yote chuoni hapo.

Morice alisema wamefanikiwa kuandaa kongamano kubwa la kisayansi na utafiti la Kairuki Annual Scientific Conference kwa mara ya tano sasa na kongamano la mwaka huu lilikuwa la kipekee kwa kuwa lilikuwa la kwanza kufanyika chuoni hapo.

Alisema serikali ya wanafunzi imefanikiwa pia kuanzisha na kusimamia vyama mbalimbali vya kitaaluma kwa kushirikiana na ofisi ya mlezi wa wanafunzi na vilabu vya kitaaluma ambavyo vimewajenga wanafunzi kitaaluma pamoja na ujuzi wa uongozi.




Uzio unaotenganisha barabara za mabasi ya mwendokasi katika eneo la Ubungo Maji, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam, ukiwa umeharibiwa. Uharibifu wa miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali, unadaiwa kufanywa na baadhi ya madereva wa vyombo vya moto wasio makini. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waadhimisha Idd kwa kuchangia damu

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

WAUMINI wa dini ya Kiislam katika Manispaa ya Mtwara Mikindani, mkoani Mtwara, wamesherehekea Sikukuu ya Eid el Haji kwa kuchangiaji damu kuwasaidia wagonjwa katika hospitali mbalimbali mkoani humo.

Uchangiaji huo umefanyika katika viwanja vya Sabasaba baada ya kumalizika ibada ya swala ya Eid Al-haji na kufuatiwa na hotuba iliyosomwa na Idrisa Bakari, ambaye ni Imamu wa Masjid Noor.

Katika hotuba yake ya Imamu Bakari aliwaasa Waislamu na Watanzania kwa ujumla kuishi kwa wema na kuwasaidia wasiojiweza, huku wakihakikisha wanakuwa chanzo cha kulinda amani isivurugike.

Alisema uislamu unatambulika kwa matendo ya wema yanayofanywa na waumini wa dini hiyo, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wagonjwa na wasiojiweza na kwamba ni wajibu wa waumini kuhakikisha utambulisho huo haupotei.

Katika hatua nyingine Imamu Bakari aliwaomba viongozi wa serikali kuzuia sherehe zenye kusababisha usumbufu na kelele kwa watu na kuzitaja sherehe hizo kuwa ni zile zinazovunja maadili ya kitanzania.

Alisema kwa sasa kumezuka tabia ya watu kukesha zaidi ya siku tatu kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu kwa madai ya kujiandaa na sherehe wanazotarajia kufanya baadaye.

# Mradi wa kuukabili umaskini watambulishwa kijijini

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa uanzishwaji wa kituo kitakachosaidia kuondoa changamoto zinazoikabili jamii hususan maeneo ya vijijini, umetambulishwa kwa wananchi wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Mradi huo ulitambulishwa na Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Erick Shigongo. Mradi huo utakaokuwa chini ya Taasisi ya Kijiji yenye makao yake katika Kijiji cha Kasisa Jimbo la Buchosa, umebuniwa na familia ya aliyekuwa Mbunge wa kwanza wa kuchaguliwa Jimbo la Sengerema kati ya mwaka 1965-1985, Hayati Alphonce Rulegura, ili kuenzi nia yake njema ya kuwawezesha wananchi wa jimbo hilo kuondokana na umaskini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo mjini Sengerema, Shigongo alisema, mradi huo utaleta faida kubwa sio tu kwa wanakijiji wa Kasisa na maeneo jirani, bali pia nje ya Jimbo la Buchosa.

"Kilichofanyika hapa leo hii ni baraka kubwa sana na nina uhakika marehemu Rulegura huko aliko mbinguni ana furaha kubwa sana, kwani jambo hili linaendeleza mema aliyokuwa akiyafanya kwa watu wa Sengerema," alisema Shigongo.

Alimpongeza Mwasisi na Rais wa Taasisi hiyo ya Kijiji, Clara Rulegura Ford, ambaye ni binti wa Hayati Rulegura, kwa kuona umuhimu wa kuendeleza ndoto za marehemu baba yake licha ya kwamba kwa sasa binti huyo anaishi na kufanya kazi Marekani.

"Ninachokishuhudia hapa leo ni fundisho kuwa watoto tunao wajibu wa kuziishi na kutimiza ndoto za wazazi wetu na kuhakikisha majina yao hayapotei kwa sisi kutenda mambo mema katika jamii tunazoishi," alisema Shigongo.

Akielezea malengo ya Taasisi ya Kijiji, mjumbe wa Bodi, Martin Rulegura, alisema ni kuchagiza suala la maendeleo endelevu katika Tanzania kupitia elimu, uwezeshaji wa jamii, wanawake na vijana.

Alisema wazo la kuanzishwa Taasisi ya Kijiji lilianza mwaka 2018 wakati mwasisi na Rais wa Taasisi hiyo, Clara akiongozana na familia yake alipotembelea kijiji cha Kasisa, mahala alikozaliwa baba yake, na kwamba alipokelewa kwa furaha na wana kijiji ambao walimweleza changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo.

"Mlinipatia risala ya mahitaji na nikaahidi ninavyoweza kusaidia na ilinichukua miaka mitatu baada ya kufanya utafiti kufikia uamuzi huu... lengo langu halikuwa kutoa fedha tu, na sasa tumefika mahala ambapo tunaweza kuanza kushughulikia changamoto zetu." Alisema Martin akinukuu hotuba ya Clara.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, ambaye aliwakilishwa na Ofisa Tarafa wa eneo hilo, Fadhili Abel, alisema kwa niaba ya serikali na wananchi wa Sengerema wanaipongeza Taasisi ya Kijiji kwa kuja na mradi huo kwani utaharakisha nia ya serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo.

HABARI KITAIFA

# DC ajitwisha zigo kero umeme viwandani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Festo Kiswaga, imelipa miezi sita Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha ndani ya miezi hiyo kunakuwa na umeme wa uhakika katika mji wa Kahama ili wawekezaji wajenge viwanda kwa wakati.

Kiswaga alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara, TRA, Mamlaka za maji, Taasisi za kifedha na kamati ya ulinzi na usalama wakati akitambulisha maonyesho ya kimataifa ya biashara na uwekezaji yanayotarajia kufanyika katika Manispaa ya Kahama, kwa lengo la kutangaza biashara zao.

Alisema ofisi yake imekuwa ikipata malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na wawekezaji juu ya kukatika kwa umeme mara kwa mara na kusababisha wawekezaji kushindwa kujenga viwanda vya uchakataji wa mazao na kuwataka kutatua changamoto hiyo mara moja.

"Nimepata malalamiko mengi tangu nimefika hapa, nishati ya umeme katika Wilaya ya Kahama ni shida, hali ambayo inafanya wawekezaji wengi kushindwa kuwekeza katika Manispaa hii...ninatoa miezi sita tatizo hili liwe limetatuliwa haraka," alisema Kiswaga.

Kiswaga alisema ukuaji wa mji wa Kahama kwa sasa ni mkubwa na lazima kuwe na viwanda vya kutosha ili wananchi wapate ajira kwa kufanya kazi na kukidhi mahitaji yao.

Nae Mwasiti Bajora, Mkazi wa Kata ya Majenga, alimpongeza mkuu wa wilaya kwa kuliona hilo, na kwamba yeye ni mjasiriamali ndogo anayesaga karanga, lakini umeme umekuwa ukikatika na kukwamisha shuhuli zake, na kwamba badala ya kukua, anazidi kudidimia kwa kukosa wateja.

Mjasiriamali Baraka Kasindi alisema wilaya hiyo ina maeneo makubwa ya uwekezaji wa wawekezaji wa ndani na nje, lakini wanashindwa kujitokeza kwa sababu hakuna umeme wa uhakika hasa katika Halmashauri za Msalala na Ushetu, ambapo ndipo kwenye maeneo makubwa.

# Wananchi wapewa huduma afya bure

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMUIA ya Isles Development Organization (IDO) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Kisiwani Pemba, imetoa matibabu bure kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa siku mbili.

Upimaji huo ulifanyika katika viwanja vya Jamhuri Wete na kuwashirikisha madaktari bingwa kutoka Unguja na wenyeji kutoka Hospitali ya Wete.

Akizungumza katika ufunguzi wa kambi hiyo sambamba na uzinduzi wa Jumuia ya IDO, Katibu Tawala wa Wilaya Ndogo Kojani, Makame Khamis, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema jambo lililofanywa IDO ni kubwa na la kuigwa.

"Niwapongeze madaktari wetu kwa uamuzi wao wa kuja kushirikiana nasi katika shughuli hii, kwani jambo walilolifanya ni sahihi na limekuja muda mwafaka,"alisema Makame.

Nae Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Yakoub Mohammed Shoka, alieleza kuwa kazi ya kutibu ni ibada, hivyo pale mtu anapomsaidia mgonjwa amefanya ibada kubwa na malipo yake yanatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mapema Mjumbe wa Jumuia ya IDO, Mbarouk Mussa Omar, alisema jumuia yao imejikita zaidi kusaidia jamii katika nyanja tofauti ikiwamo masuala ya elimu, afya, mazingira na uvuvi.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akisonga ugali wa wafungwa katika Gereza la Iringa, wakati alipofanya ziara gerezani hapo juzi. **PICHA: WMNN**.

# Simbachawene kuanza ziara Arusha, K'njaro

**Na Mwanndishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, baada ya kumaliza ziara yake ya kikazi mkoani Iringa, anatarajia kuanza ziara ya siku tano katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro ya kukagua miradi na utendaji kazi wa taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo.

Waziri huyo anatarajia kuanza ziara hiyo leo ambapo ataambatana na wakuu wa taasisi hizo.

"Lengo kuu la ziara yangu ni kuona utendaji kazi wa hizi taasisi, na pia kufanya ukaguzi wa miradi hiyo na kusikiliza changamoto zinazowakabili na kuzitatua," alisema Simbachawene.

Ataanzia ziara hiyo mkoani Kilimanjaro kwa kukagua shughuli za kiutendaji katika Chuo cha Polisi Moshi (CCP), Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Moshi (TRITA) na baadaye atazungumza na Wakuu wa Taasisi zote zilizopo ndani ya Wizara yake katika Mkoa huo.

# Shule yalia upungufu walimu wa watoto wa uhitaji maalum

**Na Kulwa Mzee**

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Kivule jijini Dar es Salaam, Kubilu Dede, amesema wana upungufu mkubwa wa walimu kwa ajili ya watoto wenye uhitaji maalum.

Amesema shule hiyo kwa sasa ina walimu wawili ambao hawatoshi kufundisha watoto 60 waliopo.

Mwalimu Dede alisema hayo wakati akiomba maboresho mbalimbali ikiwamo kuweka miundombinu rafiki katika madarasa ya watoto.

Alisema kwa sasa kuna wanafunzi 60, walimu wawili wakati wanatakiwa kila wanafunzi watano wafundishwe na mwalimu mmoja.

"Watoto tulionao ni wenye utindio wa ubongo, na walemavu wa viungo, lakini wengi ni wenye utindio," alisema.

Alisema watoto hao walianza kuwakusanya mwaka 2018 hadi 2019 na walianza na wanafunzi 15.

Akizungumzia hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kivule, Amos Hangaya alisema watoto wanahitaji darasa lenye miundombinu rafiki, vyoo, ukumbi wa kulia chakula na usafiri wa kuwafikisha watoto hao shuleni.

Alisema watoto wanapata mahitaji ya chakula shuleni, wanaingia asubuhi ambapo baadhi hadi wafatwe nyumbani.

"Wakati tunawakusanya tulikuwa tunapita nyumba hadi nyumba, wengine walikuwa wanafinchwa ndani, sisi tunawashauri wazazi au walezi wenye watoto wenye mahitaji maalum wawalete Shule ya Msingi Kivule, hakuna malipo yoyote, " alisema Amos.

Alisema hakuna mtoto aliyechagua kuwa na matatizo, hivyo walezi na wazazi wana jukumu kubwa la kuwafanya wajitegemee.

"Natoa wito kwa jamii, tunaomba mtoe taarifa kwa watoto waliopo majumbani ili wafike shuleni, kwani wakipata elimu hawatakuwa mzigo kwenye familia," alisema Amos.

# Wanawake wahamasishwa uwekezaji kwenye umeme

**Na Mary Geofrey**

WANAWAKE wametakiwa kujiamini na kujitokeza kuwekeza katika sekta ya nishati ya umeme ili kuendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, alitoa rai hiyo wakati akifungua kongamano la wanawake walio katika sekta ya nishati, lililoandaliwa na Mtandao wa Wanawake katika sekta ya Nishati Tanzania (TaWoED) na kuwakutanisha wanawake wahandisi na wanafunzi wa vyuo kwa lengo la kujadili fursa zilizopo katika sekta hiyo.

Kumbilamoto alisema kuwa umefika wakati kwa wanawake wenye uwezo katika uwekezaji hususani kwenye uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme kujitokeza na kufanya biashara hiyo kwa ufanisi.

"Nataka niwahakikishie kuwa wanawake wanaweza, na ndio maana hii leo tumeona wapo wengi waojihusisha na masuala ya uuzaji wa nishati ya umeme, kabla ya Rais hajatoa punguzo la umeme wa vijijini wa REA na mjini, sola ambayo inauzwa na kampuni za wanawake imekuwa ikisaidia jamii," alisema na kuongeza,

Alisema wapo wanawake wanaotamani kupata tenda za serikali kuu au halmashauri lakini wanakutana na vikwazo lakini kwa sababu wamejitokeza itakuwa rahisi kuwapa kipaumbele.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TaWoED, Gwaliwa Mashaka, alisema wamezindua kongamano hilo kwa lengo la kuwaleta pamoja wanawake walio katika sekta ya nishati ili kuweza kujua fursa na tenda mbalimbali zinazotolewa kupitia sekta hiyo.

Alisema mtandao huo pia utakuwa na programu maalum kwa wanafunzi waliomaliza vyuo vikuu waliosomea masuala ya uhandisi kupata elimu na kuwafundisha kwa vitendo ili kuajirika.

Kwa upande wake mshauri wa masuala ya nishati kutoka Kampuni ya Geni Energy Consulting Firm, Juliana Pallangyo, aliwataka wanawake ambao wapo kwenye sekta ya nishati ya umeme kufanya kazi kwa weledi, kujiamini na kutokata tamaa.



Mbunge wa Jimbo la Buchosa, mkoani Mwanza, Erick Shigongo (kulia), akisalimiana na Margaret Rulegura ambaye ni mjane wa aliyekuwa Mbunge wa kwanza wa Jimbo la Sengerema kuanzia 1965-1985, marehemu Alphonce Rulegura, wakati alipofika kuzindua Taasisi ya Kijiji, mjini Sengerema juzi. Taasisi hiyo itajenga kituo cha kutoa elimu ili kuchagiza suala la maendeleo endelevu katika Tanzania kupitia elimu, uwezeshaji wa jamii, wanawake na vijana. Katikati ni Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Kijiji, Martin Rulegura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa ugani washauri wakulima kufunzwa mbinu

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MAOFISA ugani wastaafu wamehimiza wakulima wafunzwe kulinda afya ya udongo, juhudi ambayo inafanywa hivi sasa kukuza matumizi ya mbole asilia ili kuinua tija katika sekta ya kilimo.

Baadhi ya maofisa ugani wastaafu wameeleza kufurahishwa na jitihada inayoofanywa wakati huu kupambana na tindikali ardhini ambayo inachakaza ardhi na kupunguza sana mavuno.

Wakuzungumzia mbolea ya kukuza kilimohai iliyozinduliwa mjini hapa, wamesifu utengenezaji wa mbolea hiyo, lakini wamehimiza pia matumizi ya mbolea zinazotokana na wanyama na mimea. Ofisa ugani mstaafu, Florence Mapunda, alisema kuna haja ya kuwaelimisha wakulimu juu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa sababu watu wengi wana elimu.

Ofisa Mstaafu, Gerald Mhagama, alipendekeza vyuo vikuu, vyuo vya mafunzo ya kilimo na taasisi za utafiti na maofisa ugani wafanye juhudi ya pamoja kuwafundisha wakulima juu ya matumizi ya mbolea. Erasto Ngole, mkulima wa parachichi mkoani Njombe, alisema kuwa alianza kutumia mbolea ya hakika toka ikiwa katika hatua ya majaribio, na kueleza kwamba kwa kutumia mbolea hiyo anavuna kutoka kwenye mti mmoja wenye afya matunda makubwa na kupata Sh. milioni 1.2.

Esther Msigwa, mkulima wa Wilaya ya Wangingombe, alisema anafarijika kuona anapata mazao mengi kwa sababu ya kutumia mbolea ya kisasa. Nina shamba ekari moja na wamenifundisha namna nzuri ya kutumia mbolea hii. Matokeo ni mazuri," alisema.

Wakala wa pembejeo za kilimo wa Rungwe, mkoani Mbeya, Daniel Mwakipesile, alisema wakulima wanaelekea kupenda mbolea ya hakika na kwamba ataendelea kuwa msambazaji wa mbolea hiyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mbolea hiyo hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Guavay ambao ndio wazalishaji wa mbolea hiyo, Mhandisi Ahad Katera, alisema wamejipanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 3,500 mpaka kufikia tani 20,000 kwa mwaka ili kukidhi mahitaji kwa wakulima.

Utafiti wa mbolea hiyo ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2017 na ulishirikisha Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Makerere, Tume ya Sayansi na Teknolojia na wadau wengine kupitia ufadhili wa Shirika la Bolnnnovate Afrika lenye makao makuu yake Nairobi, Kenya.

## Walipakodi sasa kushindanishwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga imeitaka Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa maalumu wa kikodi wa Kahama kuwashindanisha walipakodi wakubwa na wadogo ili kuwajua watu wanaojitoa katika nchi hii kwa kulipa kodi bila usumbufu.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari na kuyatambulisha maonyesho ya biashara na uwekezaji yanayotarajia kufanyika mjini Kahama kuanzia Julai 30 hadi Agosti 8, mwaka huu.

Kiswaga alisema wilaya hiyo ni moja kati ya wilaya zinazoongoza kwa kulipa kodi nchini, hivyo katika maonyesho hayo makubwa wanatarajia kuwatambua wafanyabiashara hao kwa kuwashindanisha na kuwapatia vyeti watakaoshinda.

Aidha alisema, Kahama lazima iwe na chombo cha wafanyabiashara wenye nguvu na watatambulika kwa kuona ushiriki wao katika suala zima la ulipaji wa kodi na hiyo ndio heshima kubwa kwao ambayo itaondoa malalamiko ya kufungiwa biashara zao na mamlaka.

Alisema Kahama ni soko kubwa la nchi za jirani za Rwanda, Burundi, Kongo na Rwanda, na kwamba anataka kuona Manispaa ya Kahama inakuwa jiji hapo baadaye, kwa sababu kuna wanunuzi wakubwa kutoka nchi hizo wanaonunua mahindi, mchele, karanga, madini, tumbaku na mazao mengine.

## TALGWU: Wanachama wetu wanahitaji mafunzo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), Mkoa wa Morogoro, kimeziomba Mamlaka za Halmashauri za wilaya kutoa mafunzo na elimu kwa wanachama wake kabla ya kupewa jukumu la kusimamia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki.

Katibu wa Chama hicho Mkoa wa Morogoro, Hellen Kobero, alisema hayo mbele ya Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima, kabla ya kufungua mkutano mkuu wa mkoa wa chama hicho.

Alisema kutokana na wengi kutokuwa na mafunzo na elimu ya matumizi yake, idadi kubwa ya wanachama hicho mkoa wa Morogoro wamejikuta wakipata kesi zitokanazo na upotevu wa fedha bila kujitambua.

Alisema pamoja na juhudi kubwa zilizochukuliwa na chama ngazi ya mkoa ya kuwatetea wanachama wake katika kesi mbalimbali pamoja mafanikio yaliyowezesha wafanyakazi wengi kupandishwa madaraja, bado zipo kesi nyingi za wanachama zinazosababishwa na matumizi ya mfumo huo kukusanyia mapato katika vituo.



MATUNDA YA JUHUDI ZA MIAKA 70

WHO yaitangaza rasmi China haina malaria

Ukurasa 13



Ukurasa 12

**JESHI ZIMAMOTO NA UOKOAJI 'Tumekwama maji' sakata linaloitesa vita vya moto tangu miaka ya 1970**

KUTOKA FEDHA ZA RAIS SAMIA...

# Waziri atabasamu matumizi shilingi bilioni 9.2 Hospitali ya Wazazi Meta

## •Hospitali Mkoa yaleyale, DC aishikia 'bango'

**Na Yasmine Protace**

MTU anapofika katika mikoa wa Mbeya, iwe katika zama za karibuni na simulizi ya zamani, kuna Hospitali kongwe ya wazazi ya Meta, jijini hapo.

Ina mengi imewatendea kinamama wa mkoa huo, kupitia huduma kwa kinamama, katika mwendelezo wa maboresho yake, hivi karibuni serikali imetoa Sh. Bilioni 9.2 kukamilisha hitaji lililobakia, jengo la ghorofa sita mahsusi kumhudumia Mama na Mtoto.

Wakati jengo lililobakiza asilimia 85 na linatarajiwa kumalizika Oktoba mwaka huu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amefanya ziara ya dharura kukagua maendeleo ya miradi ya afya inayoendelea mkoani humo.

Hospitalini Meta, Waziri Gwajima anakiri kufurahishwa na maendeleo hayo, akiamini upanuzi huo ni msaada kumhudumia mama na mtoto.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameshamalizia kutoa fedha zote na kufanya jumla ya Sh.bilioni 9.2 za ujenzi huu," anasema na kuongeza: "Mradi utakapokamilika, idadi ya vitanda vitaongezeka kutoka 150 hadi 400."

Dk. Gwajima anasema, ni jengo linalojitosheleza mahitaji likiwa na vitanda vya kujifungulia, vyumba vya upasuaji vinavyojitosheleza, matarajio ni kufunguliwa rasmi, Oktoba ijayo.



Waziri Dorothy Gwajima.

Jengo la Wodi ya Wazazi katika Hospitali ya Meta, jijini Mbeya, linaloendelea kujengwa kwa matarajio ya kukamilika mwaka huu. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**HOSPITALI RUFANI MKOA**

Pia, Waziri Gwajima, amekagua ujenzi wa wodi ya wahitaji wa upasuaji linalojengwa lenye vyumba sita, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

"Jengo litakuwa na vitanda 82 vitakavyolaza watu waliofanyiwa upasuaji au wanaosubiri kufanyiwa upasuaji na hii ni hatua kubwa sana kuwa na vyumba vya upasuaji sita," anasema Waziri Dk. Gwajima.

Anasema hadi sasa mamlaka ya mkoa yameshapewa Sh. bilioni tatu na wanakadiria kutumia Sh. bilioni 5.5 kumaliza ujenzi, hivyo anazitaka mamlaka mkoani kuharakisha hesabu wapatiwa fedha zilizobaki, lengo majengo yaanze kutumika mwaka huu.

"Nimefarijika kuona pia jengo la masuala yote yanayohusika na huduma za dharura kwa ufadhili wa Global Fund limekamilika." anaongeza.

**HATUA ZINGINE**

"Nimeona pia, mitambo ya oksijeni iliyounganishwa na mtambo wa kufua oksijeni ambayo imesimikwa kwenye hospitali saba za mikoa na bado tunasubiri hospitali nyingine 12.

"Huu ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na wadau wake wakiwamo World Bank na Global Fund...Kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa 'force account' hata wakija wakiangalia watafurahi, wataleta zaidi ushirikiano wa misaada mbalimbali katika kuboresha huduma za sekta ya afya," anapongeza.

**BIMA YA AFYA NA YAKE**

"Wateja wengi waje kisha muweze kunufaika na bima ya afya wanayotumia wengi kwa kuvutiwa na ubora wa huduma. Bima ya Afya sheria inakuja, Mungu akisaidia kuanzia mwakani hakutakuwapo mteja anayekuja wa msamaha.

"Kazi iliyobaki kwenu ni huduma nzuri kwa wateja na tabasamu, maana mtu mwenye hela yake anaweza kuamua kwenda zake asitumie huduma yako, iwapo haimridhishi hivyo utabaki huna wateja huku miundombinu unayo.

"Haya maslahi yetu tunayosema tunachelewa kulipwa tayari serikali imetuwekea mtaji wa miundombinu, vifaa na utaalamu tushindane kwa ubora wa huduma 'marketing' (masoko) ili tupate wateja wengi waliojiunga na bima za afya, hatimaye kusiwapo kuelemewa na misamaha.

"Wakija wengi kwa sababu wanapata huduma hapa, nanyi mtapata mapato mengi ya hospitali yatokanayo na mfuko wa bima na mkumbuke mna kamati zenu, bodi zenu, hivi atakayekuja kuwapangia ni nani, tabasamu lako hela yako, anzeni hizo sera.

**DC CHUWA AJIPANGA**

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk.Chuwa Chuwa, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa, anamhakikishia Waziri Gwajima wanasimamia maelekezo yanayotolewa na mamlaka za juu kitaifa.

"Umeona na kukagua miradi ambayo ina karibu Sh. bilioni 14 ukijumlisha. Kwa kweli, ni miradi mikubwa tunaomba upeleke salamu kwa Mheshimiwa Rais, kazi yake aliyoifanya kwa Mkoa wa Mbeya ni kubwa sana na wana - Mbeya kiujumla wanaona namna anavyohangaikia afya zao." anasema.

DK. Chuwa anasema, alishatoa maelekezo ya kufanyika kazi usiku na mchana alishaomba msimamizi kutoka Wakala wa Ujenzi nchini (TBA).

MAZINGIRA

## JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

# 'Tumekwama maji' sakata linaloitesa vita vya moto tangu miaka ya 1970

**Nimi Mweta na Christina Mwakangale**



Ndege mpya aina ya DE Havilland DASH8-400 ilipopokewa kwa saluti ya maji na Kikosi cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ikitokea Canada mwaka jana. Hayati Rais Dk. John Magufuli, aliuongoza umati. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MOJA ya maeneo yanayoleta utatanishi katika kupima mifumo ya utendaji au usimamizi wa sekta tofauti serikalini ni uwezo mdogo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini.

Ni chombo kilichobeba hadhi hiyo kuwa jeshi mwaka 1985, Bunge lilipopitisha sheria iliyoanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, hata kuifanya huduma hiyo itolewe katika nidhamu ya kijeshi, chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Pia, miaka 22 baadaye 2007, kulipitishwa sheria ya inayoboresha huduma za Zimamoto na Uokoaji nchini, iliyoviweka vikosi vya Zimamoto na Uokoaji chini ya kamandi moja, hata shughuli hiyo ikawa na sura ya kujitegemea zaidi kujiendesha.

Ndani ya mtazamo huo hadi sasa kuna uhalisia unaobaki kwamba huduma za Zimamoto na Ukoaji, ikilinganishwa na ndugu zao kama vile Polisi na Magereza, haijafikia kiwango cha mtu kulingana nao, hasa katika maeneo mawili kunakopigiwa kelele zaidi.

Kwanza siyo rahisi kufika eneo la ajali kwa wakati, kwa maana ya kuwa na gari lililosheni maji, likikimbizwa kwa gari lenye king'ora kuelekea kwenye tukio; pili uwezo wa kumaliza moto kwa nyenzo ilizoleta.

Kwanini hoja hiyo? Ni namna wanavyokwama katika tukio la kuzima moto kama sokoni Kariakoo, hoja inayodumu 'uhaba wa maji.'

**SIMULIZI YA ZAMA 1970**

Ipo picha ya marejeo zama za miaka ya 1970, iliposhuhudiwa mkasa kuungua ghala la katani katika Barabara ya Pugu (sasa Nyerere), jijini Dar es Salaam, katika eneo la viwanda vikubwa, nako kulijitokeza hoja ya kukosekana chanzo cha maji ya kutosha.

Vivyo hivyo, kuna sura ya pili iliyoacha swali, pakijulikana viwanda haviendeshwi kwa maji ya bomba ya kuchota na ndoo, bali mifumo mikubwa ya maji ya tanki katika maeneo yao.

Kiwanda hicho kiliungua kwa muda mrefu huku Zimamoto wakitafutila chanzo cha maji. Inaelekea walienda Uwanja wa Ndege ( sasa Julius Nyerere) walikopata maji.

Ujumla wake unaagukia, hadi sasa hakuna rekodi za kujitosheleza ni namna gani wahusika kwa Zimamoto na Uokoaji, wanavyokwama.

Hapo mkasa wa kilichoikuta ghala la Kiwanda cha Katani kuungua mwaka 1975, kwa maana ya miaka 46 baadaye kupitia picha ileile, kinashuhudiwa sokoni Kariakoo hakuna chanzo cha maji cha uhakika.

**MWELEKEO NI UPI?**

Utaalamu katika eneo hilo, maendeleo katika miundombinu ya maji na kudhibiti moto yanahitaji ufanisi, ikiwamo katika makao makuu ya Idara ya Zimamoto na ofisi zake zingine katika mtazamo wa kelele zinazojirudia: "haja ya kuwa na vyanzo vya maji karibu na tukio la moto."

Linabaki kuwa jambo la kawaida, hata halisikiki likijadiliwa, kwa maana ya kukumbusha umuhimu na siyo kudadisi walakini uliopo.

Kuna maelezo ya Ofisa wa Zimamoto redioni kuhusu moto hivi karibuni Kariakoo, ni kasoro katika ujazo wa gari la kuzima moto na haja ya kuwa na vyanzo jirani.

**MAHALI INAKONASA**

Uhalisi uliopo ni kwamba, inachukua wastani dakika tatu kujaza ndoo au 'dumu' la maji endapo maji bombani yanatoka kwa kasi.

Pia, ukichukuliwa mpira kuelekeza kwenye chanzo cha moto, yana kasi kubwa kumalizika, kuliko usawa wake wa kutoa maji bombani.

Mipira ya kuzimia inatajwa kuwa tofauti na kujaza ndoo bombani, suala la gari lenye mpira kujaza maji ni zaidi ya mpira wa kawaida.

Wasemaji wote wanaohusika na uzimaji moto, wanataka kuwapo vyanzo vya maji katika eneo la tukio au jirani na siyo kutegemewa safari ya kwenda na kurudi na kisha ndio kuendelea kuuzima moto.

Hali inabakia ileile ya miongo minne na nusu imevuka sasa, kuanzia Dar es Salaam iliyopita ya viwanda, ya leo imepanuka maradufu, makazi na biashara, ugumu katika zimamoto na uokoaji.

Inajenga picha kwamba, tangu uhuru wa nchi bado hakuna kituo cha Zimamoto na Uokoaji, chenye uwezo wa uhakika kujaza gari maji kwenda 'kazini' endapo wanahitajika kukabili moto mahali fulani, gari moja liapoondoka, la pili liwe linajaza maji.

Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, kinapaswa kuwa na magari na wataalamu wa kuyatumia katika namna sahihi, mathalan kujua cha kufanya endapo kuna mazingira ya upepo mkali, au mabati yanayoeneza moto kwa haraka katika mkasa.

Aidha, kuna suala la muda na taratibu za gari kuwa na maji yanayopatikana kirahisi, ukweli wake unabaki mtihani kwa Zimamoto na Uokoaji, mithili ya kuwapo zahanati yenye waganga na wauguzi, maabara, dawa na vifaa muhimu.

Hivyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, linapaswa kuwa na bajeti inayojitosheleza kuiwezesha iwajibike inapasavyo, ikiaminika bado ni kati ya maeneo wakuu serikalini 'wanazeeka' kukuna vichwa wakitafuta suluhisho kwa manufaa ya wananchi.

**SAFARI TANGU KUUNDWA RASMI 1945**

Huduma za Zimamoto Tanzania Bara, zilianza wakati wa utawala wa kikoloni baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1945. Kipindi hicho kulikuwa na kikosi kimoja tu kilichoitwa 'Police Fire Brigade' kilichosimamiwa na Jeshi la Polisi.

Miaka mitano baadaye, 1950 huduma hiyo iligawanywa katika makundi mawili, ambayo ni Zimamoto ya Manispaa iliyokuwa chini ya usimamizi wa Manispaa na Zimamoto Viwanja vya Ndege, chini ya Idara ya Kazi.

Kutokana na kupanuka miji, viwanja vya ndege na bandari, vikosi vingine vya Zimamoto vilianzishwa. Kimojawapo ni cha Bandari, ikisimamiwa na Mamlaka ya Bandari.

Mwaka 1982, huduma ya Zimamoto ya Viwanja vya Ndege, iliwekwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na vikosi vya Zimamoto vya Manispaa na Miji, viliongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, vikisimamiwa na wizara, pia tawala za mikoa na miji.

Kutokana na majukumu ya Zimamoto na Uokoaji kusimamiwa na mamlaka tofauti, ufanisi wake haukuridhisha, hata serikali ikalazimika kufanya maboresho.

Mwaka 1985, Bunge lilipitisha iliyoanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ili kuifanya huduma hiyo itolewe kwa nidhamu ya kijeshi, chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Badaaye mwaka 2007 Bunge lilipitisha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji, unaoiweka hadi sasa vikosi vya Zimamoto na Uokoaji chini ya kamandi moja.

Kwa kiasi kikubwa, ilitoa fursa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujipanga kimuundo na mgawanyo wa majukumu wenye tija ili kurahisisha utoaji huduma ya zimamoto na uokoaji.

Hadi sasa kiutawala linaongozwa na Kamishna Jenerali anayesaidiwa na Naibu Kamishna Jenerali, akifuatiwa na Makamishna watatu, wanaoongoza divisheni tatu za jeshi hilo; utawala na fedha, operesheni na tawi la usalama wa umma na mali.

Chini ya divisheni hizo, kuna vitengo vinavyoongozwa na Makamishna Wasaidizi, ili kutengeneza mfumo wa kiutendaji wenye kuleta tija katika utoaji huduma kwa jamii.

Divisheni ya Usalama wa Umma ndio hasa mahsusi linahusika na kuzuia na kukabiliana na majanga kama moto, matetemeko ya ardhi na mafuriko, pindi yanapotokea na kufanya uchunguzi wa mkasa, ili kubaini chanzo chake na kupanga mikakati ya kukabiliana nayo.

Ni divisheni inayohusika na kuelimisha jamii kuhusu majanga ya moto na uokoaji, kukagua majengo, kuzuia moto, kupanga na kukagua usalama wa ujenzi katika viwanda, vituo vya mafuta na kemikali na vituo vinavyozalisha gesi.

**INAENDELEA UK.13**




Gari la Zimamoto kwa ajili ya kuhudumia ofisi mpya, Kahama.

AFYA

MATUNDA YA JUHUDI ZA MIAKA 70

# WHO yaitangaza rasmi China haina malaria

•Uthibitisho wa miaka 4; duniani ziko 40



Mtaalamu wa China akionyesha uthibitisho, kipimo bila malaria. **PICHA: WHO.**

**Na Christina Mwakangale**

KWA mara ya kwanza baada ya kupambana na ugonjwa wa malaria kwa miongo saba, China imetangazwa rasmi na Shirika la Afya Duniani (WHO), kuwa taifa huru katika ugonjwa huo.

Huku ikiwa ndio mwasisi kwa mara ya kwanza malaria kuonekana nchini China na WHO inakuwa nchi ya 40 kutokomeza malaria kwa miaka ya karibuni ikiwamo Argentina, Algeria na Uzbekistan.

Unapozungumzia malaria, kwa nchi zinazoendelea utabaini kati ya vikwazo vikuu na visababishi vya kurudisha maendeleo nyuma, kuongeza umaskini na kupunguza nguvu kazi. Malaria huathiri zaidi mataifa ya Kusini mwa Jangwa Sahara na katika baadhi ya mataifa ya Asia na Amerika ya Kusini, mbali na ukweli kwamba ugonjwa huu, una tiba, unaepukika umeendelea kusababisha vifo vingi duniani.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema mtoto mmoja kila baada ya dakika mbili hufariki dunia, huku visa vipya zaidi ya milioni 200 vikiripotiwa kila mwaka.

Malaria ni kati ya ugonjwa unaohatarisha maisha unaosababishwa na mbu wanaoambukiza baada ya kumng'ata mtu aliyeathiriwa nakisha mwingine, huku dalili za ugonjwa zikianza kwa homa, kuumwa kichwa na tiba isiyo ya mapema inachangia vifo.

Jukumu la kukabiliana na ugonjwa huo wakati zikiendelea kutafutwa na wataalamu wa afya duniani kote, WHO wiki kadhaa zilizopita imeitangaza rasmi China nchi kutoka bara la Asia, kwamba imefanikiwa kuiondoa malaria.

**WHO INAVYOFUNGUKA**

Mbinu mbalimbali hutumika hasa kwa nchi za Afrika, ikiwamo Tanzania katika kujikinga na malaria kwa kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa (ITN), kupuliza dawa ndani na nje ya nyumba (IRS). Uzoefu wa mafanikio ya China katika kupambana na ugonjwa huo, umezua udadisi na nchi kadhaa kutaka kujifunza kufikia hatua hiyo.

WHO inasema, China baada ya miaka 70 imefanikiwa kuiondoa malaria, huku ikiwa kati ya nchi iliyowahi kukumbwa na hali mbaya sana, katika miaka ya 1940, walikuwa na mikasa milioni 30 ya malaria na tangu kipindi hicho, harakati zilianza kutafuta jibu la kukabiliana ugonjwa huo.

Shirika linasema, lilishuhudia nchi hiyo ikitumia mbinu mbalimbali katika kupambana na malaria, ikiwamo kuondoa mzunguko wa mazalia ya mbu.

WHO katika ripoti hiyo kuhusu mafanikio ya China dhidi ya malaria, limebaini kwa miaka minne sasa China haijarekodi kisa chochote cha malaria na kutangazwa rasmi, imefanikiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus, anasema mafanikio ya China hayakuwa rahisi kwa miongo kadhaa, hadi kufikia mafanikio ya sasa.

**CHINA YAFURAHIA**

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje China, Wang Wenbin, anasema kuiondoa malaria kunatokana nan chi hiyo kujali afya na haki za binadamu, huku wakijiandaa na kuandaa Sherehe ya Miaka 100 ya Chama cha China Kikomunisti (CCP), wakijivunia kutambuliwa na WHO kufikia hatua hiyo.

"CCP na serikali ya China, kila mara imeweka kipaumbele katika kulinda afya za watu wake," anasema Wenbin.

Serikali ya China ilifanikiwa kushusha kiwango cha maambukizi ya malaria kwa kutumia dawa za kujikinga za kupulizia kwenye mazalia ya mbu, sambamba na kugawa vyandarua vilivyotiwa dawa.

**MIKASA YA MALARIA**

WHO inasema, pamoja na kuwapo kinga, tiba inatolewa mara tu ugonjwa anapogundulika, inakadiriwa mwaka 2019. Matukio ya malaria duniani yalifikia milioni 229 yakiwa na vifo 409,000, (chini ya asilimia moja), huku takribani asilimia 94 ya vifo vikitokea barani Afrika.

WHO inasema, nchi inaweza kuomba kuthibitishwa kama haina malaria iwapo itaripoti miaka minne mfululizo bila ya tukio lolote la ugonjwa huo na kuwasilisha ushahidi wa kuonyesha uwezo wao katika kuzuia mikasa katika siku zijazo.

Mapema mwaka huo, chanjo iliyotayarishwa na Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza na kufanyiwa majaribio kwa asilimia 77, ikiwamo nchi ya Burkina Faso na kwamba yatazifikia nchi nne za Afrika.

**DAWA ZA ASILI**

Wanasayansi wa China, pia walitumia dawa za asili kutibu malaria miaka ya 1970 na kwamba aina ya Artemisinin, iligunduliwa kutoka kwenye mitishamba tangu karne nne.

Mtaalamu Prof. Lang Linfu, anasema ni kati ya wataalamu waliohusika kwenye utafiti na wanasayansi hao, wakibaini dawa hiyo inatibu malaria ikiwa na tatizo dogo linalotokana na athari za dawa yoyote na imeokoa mamilioni ya watu duniani.

# 'Tumekwama maji' sakata linaloitesa vita vya moto tangu miaka ya 1970

**INATOKA UK.12**

Divisheni nyingine Operesheni, mbia katika jukumu hilo la kusimamia mafunzo, kukagua huduma za zimamoto na uokoaji kwenye kanda na kufanya tahmini ya madhara kwenye majanga mbalimbali.

**ZAO LA MUUNDO MPYA**

Kupitia muundo huo tajwa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeboresha chuo chake, kufanya mapitio ya muundo wake wa ndani, kutafiti kuhusu madhara ya matukio ya majanga na kulinganisha matokeo ya ndani na nje ya tafiti hizo.

Hadi sasa inaeleza jeshi hilo limeshasambaza huduma zake kwa wananchi, kwa kuweka vituo vya zimamoto katika baadhi ya makao makuu ya mikoa, wilaya na maeneo muhimu nchi nzima.



Askari wa Zimamoto an Uokoaji, walipopambana siku kadhaa zilizopita, kulinusuru kwa moto Soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam.**PICHA: MTANDAO.**

Ni hatua inayoendana na wasifu wa kuhirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, kuongeza wigo wa utendaji. Hadi sasa, Jeshi la Magereza ni mbia wake katika kutoa mafunzo ya kijeshi ya awali, uongozi mdogo wa kati na uongozi wa juu, kuwajengea uwezo kiutendaji maofisa na askari wa Zimamoto.

Vivyo hivyo, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limekuwa karibu sana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, katika matukio ya uokoaji mkubwa.

Kwa mfano, Desemba 3, mwaka 1989 JWTZ ilishirikiana nao kukabiliana na moto uliotokea katika kampuni ya kusafisha mafuta ya Tazama Tank Farm Dar es Salaam na walifanikiwa kuuzima.

Mwaka 2001 pia vyombo hivyo vilishirikiana tena kupambana na moto wa mafuta uliotokea katika kinu cha kufua umeme yaani cha TANESCO Ubungo, Dar es Salaam Dar es Salaam na walifanikiwa kuuzima na kuokoa maisha na mali za wakazi. Maeneo mengine ni katika ajali ya meli MV Spice na MV Scagit, huko Zanzibar.

Hadi sasa inaelezwa, JWTZ limeridhia ujenzi wa vituo vya Jeshi la Zimamoto kwenye baadhi ya maeneo ya kambi zake za Lugalo, Mabibo, Kigamboni, Mbagala na Gongolamboto.

- ***Makala hii imechangiwa na sehemu ya taarifa ya historia ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.***

AFYA

# Mfuko wa Mkapa unavyopambana kujaza nafasi wazi za sekta ya afya




Hayati Rais Mstaafu, Benjamin Mkapa, alipokuwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Mfuko Benjamin Mkapa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

WALIOFUATILIA tukio la kuenziwa hayati Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, kwa kongamano lililoandaliwa na mfuko wa jina lake (BMF), walisikia takwimu ya kushangaza kuwa asilimia 70 ya nafasi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali ngazi tofauti ziko wazi.

Washiriki wa kongamano walielezwa kuwa nafasi hizo ni asilimia 50 ya nafasi zilizoko wazi katika utumishi wa umma wa jumla, hali ambayo inamaanisha kuwa serikali inajitahidi zaidi kujaza nafasi sekta nyingine kabla ya kufanya hizo sekta ya afya.

Kilichoelezwa ni jinsi mfumo huo unavyotumika kupunguza pengo hilo na siyo uwezo wa kulijaza.

Moja ya vianzio vya kutazamia kuwa pengo hilo linaweza kujazwa kwa ukamilifu kiasi fulani, ni matazamio kuwa yatakuwapo mazingira kwa vikundi na asasi huria kama Mfuko wa BejaminMkapa, ambazo kwa sehemu kubwa zina vianzio vya misaada kutoka kwa wafadhili, ili kufanya kazi zao bila matatizo.

Bado yako mazingira wezeshi kwa kiwango fulani kwa kutazamia kuwa asasi hizo zinaweza kuendesha shughuli zao kukidhi haja au matazamio, iwe kwa malengo yao wenyewe au miongoni mwa sehemu ya jamii wanayoihudumia.

Hata hivyo, mtu anaposikiliza bajeti zilizotajwa kwa mfano kwa upande wa Taasisi ya Benjamin Mkapa, siyo rahisi atazamie kuwa juhudi za asasi huria zinaweza kuziba mapengo ya wazi ya raslimali, uwezo serikalini.

Moja ya maeneo ambayo viongozi wa asasi hiyo ya Benjamin Mkapa, waligusia masuala kadhaa ya aina hiyo katika ufafanuzi wa shughuli zake katika sekta ya afya (ilianza na kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI na hasa kubadili mwelekeo wa jinsi watu wanavyoelezwa kuhusu afya zao, na ushauri unaofuata).

Rais Mstaafu Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alikiri kuwa utaalamu wa BMF uliisaidia wizara husika kubadili mwelekeo katika eneo hilo na kuwezesha 'mwito na mitikio' kuwa bora zaidi kati ya wahudumu au wataalamu sekta ya afya na wanajamii wanaohitaji huduma hizo.

Awali, kuulizia habari za maambukizi ya ukimwi ilikuwa 'sumu.' Kama ilivyo kawaida kwa sekta nyingine kama kilimo, viwanda, elimu, sayansi au teknolojia na nyingine kadhaa, suala la umuhimu unaotolewa kwa sekta ya afya liliwekewa mkazo, lakini si rahisi kusema kama serikali ingekuwa na majibu yoyote ya haraka kwa suala hilo.

**HATUA IMEPIGWA?**

Mtiririko wa takwimu, hata hivyo inaonyesha Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupunguza kasi ya vifo vya uzazi, yaani vya mama na watoto wachanga na kwa upande mwingine kuna changamoto ya utapiamlo unaoathiri watoto wa chini ya miaka mitano.

> **Moja ni kwamba, kuna vyanzo vya kiuchumi vinavyowezesha wanajamii kuungana au kuweka amana za misaada ya 'kiutu' kama sehemu mahsusi ya kile wanachokifanya, ambalo ni jambo la kawaida kwa mfano nchini Marekani.**

Viwango vya vifo kuendelea ikiwa ni zao la uduni wa akili bado vinaleta shaka. Kinachojitokeza ni kwamba , ingawa si rahisi kuweza kutajwa katika hadhara kama ile kwa mazoea, bado ufadhili hasa unaelekea kwa mashirika ya misaada ya kibinadamu (hivi sasa wapo wanaoita 'ya kiutu') ya nchi za Magharibi.

Hadi sasa ni nadra kwa mfuko kama huo kutajwa nchini. Zipo angalau mfumo kama wa Hayati Reginald Mengi, kwamba alichokifuatilia kwa nguvu hayati Mengi kimefanyiwa kazi.

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, ina mazingira ya tiba bingwa katika maeneo kadhaa, ambayo miaka 10 iliyopita ilikuwa ni ndoto kupata huduma hizo nchini.

Tatizo la kuwapo taasisi huria zenye nguvu zinazoweza kuleta mabadiliko ya haraka katika jamii, yaani kuongezea nguvu katika kile idara za serikali zinachofanya, linagusa maeneo makuu mawili.

Moja ni kwamba, kuna vyanzo vya kiuchumi vinavyowezesha wanajamii kuungana au kuweka amana za misaada ya 'kiutu' kama sehemu mahsusi ya kile wanachokifanya, ambalo ni jambo la kawaida kwa mfano nchini Marekani.

Siyo rahisi kusema barani Ulaya kuna hulka ya matajiri kuingiza fedha zao katika mashirika kama hayo, kwani ni tofauti za utamaduni kati ya Ulaya na Marekani, zinazogusa maeneo mengine, kwa mfano uchangiaji wa wazi wa matajiri kwa vyama vya siasa, ambayo ni nadra kiasi fulani barani Ulaya.

Kuna eneo ambalo mabadiliko yanahitajika ili mwelekeo huo wa kijamii kwa kupunguza au kuondoa kodi (ya mapato) kwa shughuli zenye mwelekeo huo wa kijamii.

Ni linalotajwa pia kuhusiana na kukuza vipaji vya michezo au sanaa kwa watoto wa shule za msingi na sekondari. Hivi sasa, hakuna asasi za wazi zinazojishughulisha utoaji misaada katika maeneo hayo.

Mtu anapotangaza nia ya kusaidia eneo fulani anakuwa amejipeleka mwenyewe kuwa ana fedha nyingi, anapaswa kuanza kufuatiliwa ulipaji kodi wake, hata kuifanya jamii kujinasibu na ukwasi ulio nao.

Eneo jingine linatajwa kuwa uduni wa taasisi za wakfu katika jamii. Imezoeleka kwamba, mali za mtu binafsi na pale anapofariki wanagawana, na si dhihaka kusema kuwa kifo cha mtu mwenye fedha kinafuatiwa na 'arobaini' ya unywaji pombe miongoni mwa wanae.

Kulingana na ukwasi wa mtu huyo, fedha zikipungua ndiyo vijana hao wanaanza tena kuhangaika kama walivyozoea, baada ya kupoteza mamilioni ya fedha ambazo zingeingia katika mifuko ya kuongeza huduma za jamii kwa mfano katika afya, elimu na sanaa.

Ni kielelezo cha udhaifu wa mshikamano katika jamii na ni sababu isiyo ndogo ya wazee wasiojiweza kunyanyaswa wanapokwenda kufuatilia mafao, au kwenda hospitalini bila fedha ya kununua dawa.



# Vikundi 1,000 Chamwino vilivyonufaika TASAF

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WALENGWA 14,167 wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kutoka vikundi 1,077 wilayani Chamwino wamefanikiwa na uandaaji wa mipango ya biashara ili kujiinua kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Athuman Masasi, aliyasema hayo juzi kuhusu utekelezaji wa mpango huo.

Alisema mipango hiyo imeshapitishwa katika ngazi ya Halmashauri na kuwasilishwa TASAF makao makuu ili walengwa hao wawezeshwe zaidi ya Sh. milioni 5.7.

Masasi alisema fedha hizo zitawasaidia walengwa katika kuendesha shughuli zao mbalimbali za kimaisha ikiwamo wengine kuibua biashara ndogo ndogo ili kujikwamua kiuchumi.

"Walengwa wamekuwa wakipewa elimu kabla ya kupewa fedha hizo, ili kuhakikisha wanajiandaa kujiinua kiuchumi kupitia fedha za TASAF wanazopata," alisema Masasi.

Alisema jumla ya miradi 112 imeibuliwa Juni mwaka 2021 kwa ajili ya kutekelezwa kwa mwaka 2021/22.

"Miradi hii imetumwa TASAF makao makuu kwa ajili ya uhakiki kabla haijaanza kutekelezwa na aina ya miradi iliyoibuliwa ni pamoja na uchimbaji wa malambo, ujenzi wa barabara za jamii, visima vifupi na upandaji miti."

"Hiyo ndio miradi ambayo imeibuliwa katika kipindi hiki, bado tunaendelea kuitekeleza," alisema Masasi.

Kadhalika, alisema mafanikio ya utekelezaji wa mpango huo ni kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto shuleni na vituo vya afya, walengwa wameanzisha bustani za mboga , hususani kwenye mabwawa yanayohifadhi maji kwa muda mrefu.

Alisema walengwa wengi wamejenga hali ya kujiamini kiasi cha kuchaguliwa viongozi kwenye maeneo ambayo wanaishi.

Hata hivyo, alisema katika vikundi vilivyoundwa walengwa wengi wamepanga kuendesha biashara ambazo wanaamini hapo baadae zitawasaidia katika kujiendeleza.

Alisema Wilaya ya Chamwino imekuwa ikijenga uwezo kwa walengwa wa TASAF III kwa njia ya mikutano semina pamoja na mikusanyiko mbalimbali ili kupata uwelewa wa kutosha kuhusiana na fedha za TASAF ambazo wanapatiwa.

# RC Mtaka aombwa kibano kwa wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuzuia wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kwenda kwenye kumbi za starehe na baa nyakati za masomo, kwa kuwa ni chanzo cha kufeli.

Ombi hilo lilitolewa na mwalimu wa Shule ya Sekondari ya DCT Mvumi, Janken Hosea, kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kwenye kikao cha wakuu wa shule na wakuu wa idara za shule zinazomilikiwa na Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT).

Mwalimu Hosea alisema chanzo cha kiwango cha ufaulu kushuka kwa wanafunzi ni kutokana na kutokana na kuonekana kwenye kumbi za starehe.

Kufuatia ombi hilo, Mtaka alisema moja ya mikakati ambayo serikali imeweka ni kuhakikisha wanafunzi wa rika hilo hawaonekani katika maeneo hayo muda wa masomo.

"Pamoja na mikakati hiyo, lakini wazazi nao wanapaswa kukemea suala hili kwenye familia zao, lengo ikiwa ni kutekeleza mkakati wa kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi."

"Katika hili naomba sote tushirikiane kwa sababu wazazi pia mnapaswa kushirikiana ili kuhakikisha wanafunzi wananyooka katika hilo," alisema Mtaka.

Alisema lengo ni kuona wanafunzi wa shule za Mkoa wa Dodoma zinakuwa bora katika ufaulu wa mitihani mbalimbali ya kitaifa na mingine.

Aliwataka viongozi wa shule hizo kutenga muda wa kwenda kujifunza katika shule ambazo zinafanya vizuri kitaaluma katika mitihani ya kitaifa na mingine ili kupata mbinu za kuongeza ufaulu.

Mtaka alisema wasione aibu kwenda kujifunza namna ya shule hizo zinafanya vizuri hususan zinazoingia kumi bora kitaifa kila mwaka.

"Baba Askofu tengeni muda na kuchagua shule mbili ambazo ni best (bora) katika ufaulu ili waende kujifunza na baadae shule zao nazo waje waige mikakati ya kufanya."

"Kuna shule kama St. Francis kila mara iko kweye kumi bora, mnapaswa kuwauliza wanafanyaje mpaka wanafikia huko," alisema.

Naye Askofu wa Kanisa hilo Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, aliahidi kuyafanyia kazi yote aliyoelekeza Mkuu wa Mkoa ili kuinua kiwango cha elimu.

Aidha, aliwataka wakuu wa shule hizo kuitisha kikao cha pamoja kwa ajili ya kujadili kero za kielimu, lakini kujadili namna ya kutekeleza maagizo ya mkuu wa mkoa.



Mratibu wa Miradi kutoka Taasisi ya Restless Development, Benetius Boniphace (kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalanganya, katika kongamano la kuwajengea uwezo vijana ili wajiajiri na kuajirika kukabiliana na tatizo la ajira nchini, lililofanyika jijini humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: PAUL MAABEJA**

# Rushwa yatajwa saratani kwa maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema rushwa ni saratani kubwa inayokwamisha maendeleo kwa wananchi.

Jafo alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifungua semina kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma walio chini ya Klabu ya kupinga rushwa (UDOSOAC), ambayo iliandaliwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema vitendo vya rushwa vinasababisha wananchi washindwe kupata huduma za kijamii, hivyo kuchangia ukiukaji wa haki za msingi wanazostahili kuzipata.

Waziri Jafo aliongeza Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kwa wananchi lakini zinaingiliwa na vitendo vya rushwa hali inayosababisha ijengewe chini ya kiwango.

"Ndugu zangu, leo hii mkandarasi akipewa dhamana ya kujenga barabara ya kilomita 10 na upana wa mita 7. 5 na kwa vile kuna mazingira ya rushwa msimamizi wa mradi yuko site atashindwa kumsimamia mkandarasi huyo na atajenga chini ya kiwango," alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Faustine Bee, alitoa rai kwa kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua.

Alisema rushwa ya ngono ni changamoto kubwa katika vyuo hapa nchini na kuongeza kuwa mapambano dhidi ya vitendo hivyo yameshirikisha vijana wa vyuo kwa kuwa ndio wanakumbana navyo.

"Nawaomba vijana wote acheni kabisa kujihusisha na vitendo hivi vya rushwa, katAeni kupokea au kutoa rushwa kwani tunataka vyuo vyetu visonge mbele," alisisitiza.



# TFS yakabidhi madawati 200 shule za Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** RUGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imekabidhiwa madawati 200 na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), kupitia shamba la miti la Kiwira ili kutatua kero ya uhaba wa samani hizo kwenye shule mbalimbali.

Akikabidhi madawati hayo juzi, Mhifadhi Mkuu wa shamba la miti Kiwira, Lucas Sabida, alisema madawati hayo ni kwa ajili ya shule za msingi za kata mbili za Igoma na Isongole ambazo zinalizunguka shamba hilo na kila kata imetengewa madawati 100.

Alisema uongozi wa TFS uliamua kutoa msaada huo kwa sababu wananchi wa kata hizo ndiyo wanaoshirikiana na uongozi wa shamba hilo kulinda miti dhidi ya uhalifu wa aina mbalimbali ikiwamo uchomaji moto.

Alisema madawati hayo yatasaidia wanafunzi 600 ambao walikuwa wanasongamana kwenye madawati machache kuondokana na tatizo hilo ambalo limekuwa likiwasababishia kusomea katika mazingira magumu.

"Tuna shughuli nyingi za uendeshaji wa shamba hili ambazo tumekuwa tukishirikiana na wananchi wa vijiji vyote vinavyotuzunguka, wamekuwa wakishirikiana nasi kukabiliana na moto, kupunguza miti na hata kwenye utunzaji wa vitalu kwa hiyo tumeona ni vyema tuwasaidie watoto wetu madawati haya," alisema Sabida.

Alisema uongozi wa shamba hilo utaendelea kushirikiana na wananchi hao kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ili kuendeleza uhusiano mwema ambao unalifanya shamba kuendelea kulindwa muda wote.

Akipokea madawati hayo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo pamoja na wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuulinda msitu huo ikiwamo kuzuia moto ili waendelee kufaidi matunda.

Alisema msitu huo ni mali ya serikali mtu yeyote atakayefanya shughuli za kuuhujumu atachukuliwa hatua kali za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo haramu.

Alisema kutokana na faida ambazo wananchi wanaozunguka msitu huo wanapata sawa na ni wa kwao pia wana wajibu wa kuulinda.

Alisema madawati hayo ambayo uongozi wa TFS umeikabidhi serikali yatasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa madawati katika wilaya hiyo.

"Haya madawati ni mengi sana, tungetaka kuwachangisha wananchi fedha zingewatoka nyingi sana, sasa tumeshaona matunda hivyo mtu asirogwe aje kuhujumu msitu huu, hatuombei mtu afanye uhuni, lakini ikitokea tutashughulika naye kwa nguvu zote," alisema Dk. Anney.

Diwani wa Kata ya Isongole, Mwalongo Sote, alisema wakala huo pia unashirikiana na wananchi kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati na miundombinu mingine.

Alisema kutokana na michango hiyo wananchi wameanza kuona msitu huo ni mali yao na wanalinda kwa kuzuia mambo mbalimbali ikiwamo ujangili ambao ulikuwa kero miaka ya nyuma.

Naye Diwani wa Kata ya Igoma, Andrew Mwaipopo, alisema ushirikiano wa msitu huo na wananchi haujawahi kutokea katika eneo lolote kwa sasa hata ulinzi wa msitu huo umekuwa rahisi kuliko ilivyokuwa awali.

Alisema katika kata yake vijana wengi wameajiriwa kufanya shughuli mbalimbali za msitu huo ikiwamo kupunguza miti na kupanda.




Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Dk. Vincent Anney (kulia), akipokea msaada wa madawati 200 kutoka kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Kiwira, Lucas Sabida, kwa ajili ya shule za msingi za kata zinazozunguka shamba hilo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Matumizi ya vyoo bora yaongezeka kwa wananchi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MATUMIZI ya vyoo bora mkoani Mbeya, yameongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2017 hadi 76, mwaka huu hali iliyochangiwa na kampeni mbalimbali zilizoendeshwa na serikali pamoja na wadau.

Ongezeko hilo limechangia kuwaepusha wananchi na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu ambacho kilikuwa kinasumbua miaka ya nyuma hasa kipindi cha masika.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Mbeya, Mashaka Juma, aliyasema hayo juzi wilayani Chunya wakati wa kukabidhi vifaa vya kisasa vya ujenzi wa vyoo katika shule za wilaya hiyo vilivyotolewa na wadau mbalimbali.

Alisema kwa sasa elimu ya afya imesambaa mpaka maeneo ya vijijini hali ambayo imesababisha idadi kubwa ya wananchi kuanza kuzingatia ujenzi wa miundombinu hiyo na kuitumia.

"Kipindupindu lilikuwa tatizo kubwa sana miaka ya nyuma kutokana na idadi kubwa ya watu kutotumia vyoo, sasa hivi elimu imesambaa vya kutosha na sasa tumefikia kiwango kikubwa sana kitaifa, sasa tumeanza kusahau kipindupindu," alisema Mashaka.

Alisema Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya ambazo zilikuwa zina tatizo kubwa la vyoo, lakini sasa hivi tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa.

Baada ya kupokea vifaa hivyo baadhi ya walimu wa shule za msingi za wilaya hiyo ambazo zitanufaika na msaada huo, waliwashukuru wadau waliojitolea kwa maelezo kuwa vifaa hivyo vitasaidia wanafunzi kujisitiri.

Mmoja wa walimu, Agneta Nchimbi ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chunya Mjini, alisema kukosekana kwa vyoo bora shuleni baadhi ya wanafunzi huwa wanalazimika kutoroka shule na kwenda kujisaidia nyumbani.

Aliahidi kuwa watahakikisha wanalinda miundombinu hiyo ili itumike kwa muda mrefu na kukuza kiwango cha elimu katika shule yake kwa kuongeza ufaulu.

# Watanzania wakumbushwa kujenga umoja

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wametakiwa kujenga umoja imara bila kujali tofauti ya dini zao na itikadi za kisiasa ili kuliepusha taifa na migogoro inayoweza kukwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya afya, elimu na sekta zingine.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalabaa, aliyasema hayo jana wakati wa Baraza la Idd El Adha ambalo kimkoa lililofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya na kuwashirikisha waumini wa dini ya Kiislam pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali.

Aliwataka viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa ili liendelee kuwa na amani na mshikamano pamoja na kuwaombea viongozi mbalimbali wa serikali ili waliongoze taifa kwa kuzingatia misingi ya haki.

"Pia sisi viongozi wa dini tunatakiwa tuliombee taifa letu ili Mwenyezi Mungu atuepushe na janga hili la corona ambalo linatishia dunia, sisi ndiyo chachu ya maendeleo hivyo tunatakiwa tuwahamasishe wananchi kujikinga," alisema Shekhe Njalabaa.

Alisema ukosefu wa amani katika taifa lolote ni miongoni mwa vikwazo vya maendeleo na kuwasisitiza Watanzania kila mmoja kwa imani yake aliombee taifa amani na utulivu pamoja na kushiriki kuzuia vitendo vya uvunjifu wa amani.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye baraza hilo akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema ameshatoa maelekezo kwa viongozi mbalimbali wa serikali kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuepuka ugonjwa huo na kuwaomba viongozi wa dini pia kushiriki kwenye utoaji huo wa elimu kwa waumini wao.

Alisema ugonjwa huo kwa sasa ni tishio duniani kote na tayari katika mkoa huo kuna wagonjwa ambao wanaendelea kupata matibabu kwenye vituo mbalimbali vilivyotengwa.

"Nashukuru nimeona baadhi mmevaa barakoa ili kujikinga na janga hili, sasa nawaombeni tushirikiane kutoa elimu ili wote tuwe tunajikinga, hakikisheni mnanawa mikono mara kwa mara kwa kutumia maji tiririka na sabuni au tumia vitakasa mikono," alisema Dk. Chuachua.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, aliwapongeza viongozi wa Baraza la Idd kwa kuwaalika viongozi wa dini zingine kuwa utaratibu huo unasaidia kuchochea mshikamano miongoni mwa wananchi.

Dk. Tulia ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kuchangia mifuko 200 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Waislam (BAKWATA) mkoani humo.

Vilevile, alisema Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliahidi kuchangia Sh. 2,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizo na alitakiwa kuwapo lakini alishindwa kutokana na kuwa ziarani katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.



# Dk. Mwinyi ashiriki Eid Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amejumuika pamoja na Waislamu katika ibada ya swala ya Eid-Elhajj iliyoswaliwa katika viwanja vya Mnazimmoja, Wete mkoani Kaskazini Pemba.

Waislamu duniani kote husherehekea Sikukuu ya Eid - Elhajj baada ya kumaliza kutekeleza kwa ibada tukufu ya Hijja huko Makka ambayo huambatana na kuchinya wanyama kama ng'ombe, mbuni, kondoo na ngamia.

Akitoa hotuba baada ya kumaliza swala hiyo, Sheikh Abdulrahman Hilal, alisema lengo la kuwapo kwa ibada ya Hijja ni kithibitisho cha imani ya mja na kuwa karibu na Mola wake.

Alisema kuwa katika ibada ya Hijja kuna manufaa yanayopatikana ndani yake na huwaweka Waislamu pamoja kushirikiana na kuleta usawa kwa watu wote.

"Upendo na mshikamano ni kitu kizuri sana na ni muhimu ambacho kinapatikana kwa Waislamu, hasa pale kunapokuwa na kitu cha kuwaweka pamoja ikiwamo kwenye swala," alisema.

Alisema Allah anawatakia waja wake mepesi, hivyo ni vyema kwa kila Muislamu mwenye uwezo, kwenda kutekeleza ibada tukufu ya Hijja kwa chumo la halali ili ibada zake zikubaliwe.

"Haitakiwi kuhiji kwa chumo la haramu, hivyo Waislamu mtambue kwamba kila anayetaka kwenda kutekeleza ibada hiyo, lazima mali yake iwe ya kuchumwa kwa njia halali," alionya.

Alisema kitabu kitukufu cha Quran kinabainisha mtu bora ni anayemcha Allah, hivyo kila Muislamu ahakikishe kwamba anatekeleza yale yote aliyoyaamrisha na kuacha yale yote aliyoyakataza Mwenyezi Mungu.

Alisema ni mwaka wa pili sasa Waislamu wa nchi mbalimbali wanakosa kwenda kwenye ibada ya Hijja kutokana na dunia kukabiliwa na janga la ugonjwa wa corona.

"Kila mwenye nia ya kwenda kuhiji basi Allah atamfanyia wepesi, kwani Allah anawapenda waja wake na anawatakia mema," alisema.

Sheikh huyo aliwataka kinababa kuwa karibu na familia zao na kinamama kuwa waangalifu kwa watoto wao, ili kuepukana na matatizo yanayoweza kujitokeza.

"Ni wajibu kwa kila baba kuwa karibu na familia yake hasa katika kipindi hiki cha sikukuu kwani kunaweza kujitokeza uhalifu," alisema.

Katika swala hiyo viongozi mbalimbali wa kitaifa walihudhuria akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Massoud, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdalla na viongozi wengine wa vyama vya siasa na serikali.

## 'Wazazi waongeze ulinzi kwa watoto'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Zanzibar inaungana na mataifa mengine ulimwenguni kusherehekea sikukuu ya Eid-Hajj, Mkurugenzi wa TAMWA-Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanaongeza ulinzi kwa watoto wao katika kipindi chote cha sikukuu.

Alisema jana kuwa Zanzibar kama sehemu nyingine za dunia, watoto husherehekea sikukuu kwa kwenda maeneo mbalimbali ikiwamo kuwasalimia ndugu na kwamba wapo watu wenye nia ovu hutumia mwanya huo kutimizia dhamira zao mbaya zikiwamo za kuwadhalilisha watoto kijinsia.

Alisema kusherehekea sikukuu ni jambo zuri ambalo huleta furaha kwa watoto na wazazi wao, lakini furaha hiyo inapaswa kuwekewa umakini zaidi ili isigeuke kuwa sehemu ya majonzi.

Alisema watu wenye nia ovu huishi karibu na jamii, hivyo ni rahisi kuwaona watoto wanaotembea mitaani na kuwahadaa ili kuwafanyia udhalilishaji wa kijinsia.

Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha hawawaachi watoto wao kwenda kwenye viwanja vya sikukuu peke yao, badala yake waongozwe na watu wenye kuaminika.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanaacha tabia ya kuwavalisha watoto nguo zisizozingatia maadili.

Sambamba na hayo, aliliomba Jeshi la Polisi katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba kuongeza ulinzi kuanzia barabarani ili kuepusha ajali za watoto zinazoweza kuepukika sambamba na maeneo yote ya viwanja vya sikukuu.




Meneja Masoko wa Zantel Zanzibar, Rukia Mtingwa (kushoto), akifurahia jambo na mgunduzi wa teknolojia, Said Sugu, wakati wa uzinduzi wa kijiji cha kidigitali ambacho ni maalumu kwa ajili ya watu kujifunza matumizi ya mtandao wa 4G, jijini Zanzibar jana. Kulia ni mbunifu wa teknolojia Soud Hassan. Wagunduzi hao wamefanikisha kutengeneza vitu mbalimbali ikiwamo helikopta na magari wakitumia kipaji na intaneti kama nyenzo ya kujifunzia. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Zantel wazindua kijiji cha kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya simu ya Zantel imezindua kijiji cha kidigitali, kikiwa ni eneo ambalo limewekwa miundombinu imara ya intaneti kwa lengo la kutoa mafunzo kwa wakazi wa Zanzibar namna bora ya kutumia mitandao katika kujiendeleza kielimu na kibiashara.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa kampeni yao ya 'Pasua Anga kiZantel 4G' awamu ya pili, ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kutoa elimu kwa wakazi wa Zanzibar juu ya umuhimu wa mtandao wa 4G katika kuleta maendeleo ya kijamii na uchumi.

Mpango huo ni sehemu ya mkakati wa Zantel wa kuchochea mageuzi ya kimtandao na kufanya watu waishi kidigitali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja Masoko wa Zantel-Zanzibar, Rukia Mtingwa, alisema kituo hicho kitatoa huduma za kimtandao bure kwa wakazi wa Zanzibar ndani ya miezi miwili.

"Sehemu hii ina wataalamu na wabobezi wa huduma hizo za elimu na biashara za mtandaoni ambao watakuwa wakitoa mafunzo kwa watu watakaofika hapa," alisema.

Meneja huyo aliendelea: "Elimu ya mtandaoni si kwa ajili ya wanafunzi wa shule na vyuo tu, bali hata kwa watu wenye vipaji mbalimbali na wafanyabiashara wanaweza kujifunza kupitia mtandao namna bora ya kukuza na kutangaza kazi zao na kuboresha.

"Kwa mfano leo hii tuko na Said Sugu ambaye yeye ameweza kutengeneza magari, helikopta kwa kutumia kipaji chake na mtandao kuongeza ujuzi."

Alisema wafanyabiashara pia wana fursa ya kupata masoko mapya mtandaoni na kwamba wakiwa katika kijiji cha kidigitali, watafundishwa namna rahisi ya kutumia mitandao kuuza na kutangaza biashara zao.

Pamoja na hilo, Zantel imezindua shindano la kidigitali ambalo linatoa fursa kwa watu mbalimbali kuonyesha vitu ambavyo wamejifunza na kutengeneza kwa kutumia mtandao na kujishindia zawadi hadi Sh.300,000.

"Unachotakiwa kufanya ni kutengeneza video fupi na kuiweka kwenye mtandao wa kijamii na kutag kurasa za Zantel. Video ambayo itapendwa zaidi itajishindia zawadi hadi Sh. 300,000," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA ZINAUZWA

NYUMBA ZIPO 3 KATIKA ENEO MOJA MAHALI KIBAHA MAILI MOJA UKUBWA 25M X 25M INAVYUMBA 11,VYUMBA 7 VINAJITEGEMEA NA CHUMBA NA SEBULE VIWILI,INATYLES,MADIRISHA ALUMINIUM NA BATI LA MSOUTH,MAJI NA UMEME VIPO,DOCUMENT MAUZIANO YA SERIKALI ZA MITAA

**MAWASILIANO:0768 909866**

## NYUMBA INAPANGISHWA

NYUMBA INAPANGISHWA INA VYUMBA VINNE KIMOJA MASTER BEDROOM, IPO MAENEO YA MWENGE NZASA, INA MAJI NA UMEME ,IPO NDANI YA FENCE(UKUTA)

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**PIGA SIMU NAMBA:0682 600 101**

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 51/2019**
**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA JINAI NO. 280/2017**
**MKURUGENZI WA MASHITAKA...........MRUFANI**
**DHIDI YA**
**AFANA SHAIBU MBILAMBI...........MRUFANIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA: AFANA SHAIBU MBILAMBI – LIKOMBE MTWARA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe **26/07/2021 saa 2:30** asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo **tarehe 14/7/2021.**

116367602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 37/2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 119/2018, Mahakama ya Wilaya Lindi)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA.......................................MRUFANI**
**Dhidi ya**
**MOSES JAPHET@ MGENI...............MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: MOSES JAPHET @ MGENI – NZOVWE MBEYA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 28/07/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03/06/2021.

116367702

**PUBLIC ANNOUNCEMENT TO CLOSE THE COMPANY**

THE SHAREHOLDERS OF BELFORD INVESTMENT LIMITED (REGISTRATION NO 68716 DATED 26TH NOVEMBER 2002 IN ACCORDANCE WITH THE COMPANIES LAWS AT BRELA WISH TO SHUT DOWN THE COMPANY OPERATION DUE TO CIRCUMSTANCES THAT ARE BEYOND OUR CAPABILITY.

116364802

**IMARA BRAKE LININGS TABATA DAMPO**

**MALI MPYA IMEWASILI.**

**Gundi (Bostik) kwa Sh. 130,000/- Kwa ujazo wa lita 5.**

**Wasiliana nasi kwa simu namba 0783 277 909; 0714 475 898.**

116367002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**SHAURI LA NDOA/TALAKA NO. 35/2021**
**MDAI...........ARMSTRONG WILIAM MCHOME**
**MDAIWA...........NEEMA GODWIN MWAIFUGE**

Kwa mdaiwa mtajwa hapo juu. Popote pale ulipo unatakiwa kuhudhuria Mahakama ya Mwanzo Chalinze Bagamoyo bila kukosa **tarehe 28/07/2021** siku ya Jumatano saa 2:30 asubuhi kujibu madai yako.
Tambua kuwa kutofika kwako shaurini Mahakama itaanza kusikiliza shauri hilo upande mmoja na maamuzi yatatolewa bila wewe kuwepo.

**Imetolewa leo tarehe 16/07/2021**

116368502

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA EID AL ADHA KATIKA PICHA



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu wakishiriki swala ya Eid Al Adha katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya kinamama wa dini ya Kiislamu wakishiriki kwenye swala ya Eid Al Adha katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa nyama kwa Adija Kondo, uliyotolewa na Taasisi ya Muslim World League, jijini humo jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo hapa nchini, Hassan Katungunya. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waumini wa dini ya Kiislam mjini Iringa wakichinja mbuzi jana, zilizotolewa na taasisi mbalimbali nchini na nje ya nchi kwa taasisi ya Dhi Nureyn, kwa ajili ya kusaidia yatima, wazee na watu wasio na uwezo kusherehekea sikukuu ya Eid Al Adha. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislam mkoani Mtwara, wakichangia damu jana, kama sehemu ya maadhimisho ya Eid Al Adha. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**



Baadhi ya Waislam wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakishiriki chakula nyumbani kwa Diwani wa Kata ya Majengo, Mukadamu Sabuni (aliyesimama kulia), kama sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Eid Al Adha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# ARSENAL yasitisha safari ya Marekani



**LONDON, England**

ARSENAL imejiondoa kwenye safari ya kwenda nchini Marekani kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya kutokana na ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona kwa baadhi ya watu waliotakiwa kwenda nao, leo Alhamisi.

Washikabunduki hao walitakiwa kushiriki kwenye mashindano ya Kombe la Florida kwa kucheza dhidi ya Inter Milan hapo keshokutwa na Everton au Millonarios Julai 28, mwaka huu, mjini Orlando.

Arsenal ilisema katika taarifa yake kwamba "maamuzi magumu" yalifanywa kwa ajili ya kuhakikisha afya ya wachezaji wa klabu na benchi lake la ufundi.

"Tunaelewa kwamba, hali hii imewakatisha tamaa mashabiki wa Marekani ambao walikuwa wanatusubiri kutuona kwenye Kombe la Florida, ikiwa sehemu yetu ya maandalizi," ilisema taarifa hiyo.

"Tunaomba radhi kwa waandaji wa michuano ya Kombe la Florida ambao wamefanya kazi ya kuvutia kwenye maandalizi.

"Hivyo tumelazimika kusitisha safari hii, kutokana na ongezeko la maambuzi ya virusi vya corona kwa baadhi ya watu wetu ambao tulipanga kwenda nao Marekani.

"Afya ni jambo la msimu zaidi, hivyo tumelazimika kufanya uamuzi mgumu wa kusitisha safari hii."

# PSG YAJITOSA KUMWANIA POGBA



**MANCHESTER, England**

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola anajadiliana na Paris Saint-Germain juu ya uwezekano wa uhamisho wa mteja wake huyo, limedai gazeti la Daily Mail.

Pogba katika mkataba wake wa sasa na United amebakiwa na mwaka mmoja huku mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya yameshindikana.

Baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye michuano ya Euro 2020 akiwa na Ufaransa, kiungo huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa.

Timu yake ya zamani ya Juventus nayo imekuwa ikiwania kumrejesha kule Turin na sasa PSG nao wametia mguu wao.

Pogba kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka United, lakini sasa dili hilo linaonekana kuwa njiani kukamilika.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Man United inahisi presha kubwa ya kumpoteza mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ambaye atakuwa huru baada ya miezi 12 ijayo.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo PSG wanajadiliana na Raiola juu ya uwezekano wa uhamisho utakaogharimu kiasi cha pauni milioni 43 ili kuondoka hapo kwa mashetani wekundu.

Kiasi hicho cha fedha ni nusu ya kile walicholipa Man United mwaka 2016 wakati wakimsajili kutoka Juventus.

# Henderson atingisha kibiriti Liverpool

**LIVEROOL, England**

JORDAN Henderson anakaribia kuondoka katika kikosi cha Liverpool baada ya mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya kukwama, kwa mujibu wa gazeti la Dail Mail.

Henderson bado ana mkataba wa miaka miwili hapo kwenye dimba la Anfield, lakini anataka kuongezewa mpya, lakini dili hilo linaonekana kushindikana.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, mchezaji huyo yupo tayari kuondoka klabuni hapo kama hatapewa nyongeza ya mkataba mpya.

Gazeti la Athletic liliripoti mapema wiki hii kwamba, kocha wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino amekuwa akimwania sana kiungo huyo.

Ripoti hiyo imebainisha kwamba, kwa sasa PSG wanafanya jitihada za kutaka kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa England.

Liverpool tayari imeshampoteza Georginio Wijnaldum aliyeondoka kama mchezaji huru kwenda kujiunga na PSG mwezi uliopita.



HABARI MICHEZO

# Broja ajifunga Chelsea hadi 2026

**LONDON, England**

ARMANDO Broja amesaini mkataba wa muda mrefu na klabu ya Chelsea ambao utamweka hapo Stamford Bridge hadi mwaka 2026.

Mshambuliaji huyo raia wa Arbania, ambaye atafikisha umri wa miaka 20 Septemba mwaka huu, alikuwa akiendelea katika timu ya vijana na alicheza mchezo wake wa kwanza na kikosi cha kwanza akitokea benchi dhidi ya Everton Machi, 2020.

Alitumia msimu uliopita kwa mkopo huko Vitesse Arnhem, akifunga mabao 11 katika mechi 34 kwa timu hiyo ya Ligi Kuu ya Uholanzi.

Uhamisho wa Olivier Giroud kwenda AC Milan, ambao ulikamilishwa Jumamosi na uvumi unaounganisha Tammy Abraham naye kuondoka hapo Stamford Bridge inamaanisha Broja anaweza kuwa katika mipango ya kocha Thomas Tuchel kwa msimu wa 2021-22.

"Nimefurahi sana kusaini mkataba mpya na Chelsea. Baada ya kupitia akademi ya hapa ilikuwa wakati maalum kwangu kucheza kikosi changu cha kwanza mwaka jana, kabla ya kupata uzoefu zaidi kwa mkopo kule Vitesse msimu uliopita," alisema akiiambia tovuti rasmi ya Chelsea baada ya kusaini mkataba huo.

Chelsea wataanza kampeni yao ya Ligi Kuu nyumbani dhidi ya Crystal Palace Agosti 14, mwaka huu, ambapo ni siku tatu baada ya kucheza na Villarreal kwenye UEFA Super Cup huko Belfast.

Mchezo huo unamkutanisha bingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na mshindi wa Kombe la Ligi ya Europa.



# JUVENTUS yajitoa kumwania Jesus




**TURIN, Italia**

JUVENTUS imejiondoka kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili, Gabriel Jesus baada ya klabu yake ya Manchester City kutaja bei ya nyota huyo.

Juventus inaaminika ni klabu iliyokuwa inavutiwa sana na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kwa muda mrefu, lakini sasa City wametaja dau lake ni pauni milioni 43.

Baada ya kuondoka kwa Sergio Aguero kwenda Barcelona, Jesus ndiye mshambuliaji pekee mwenye uzoefu mkubwa pale aliyebakia City, ingawa Kocha Pep Guardiola hakuwa akimchagua sana kwa msimu uliopita.

Lakini mpango wa nyota huyo kuondoka City unaonekana kuwa mgumu kidogo, baada ya Juventus kuripotiwa hawawezi kulipa dau lililowekwa na klabu yake.

Jesus amefunga jumla ya mabao 82 katika mechi 195 tangu alipowasili klabuni hapo, na kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu England (EPL).

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, alitumia likizo yake ya kimataifa kuisaidia Timu ya Taifa ya Brazil kupambana kwenye Copa America, lakini alizikosa mechi za nusu fainali na fainali.

# LAMELA KUPISHANA NA GIL SPURS

**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur na Sevilla wapo njiani kukamilisha dili la uhamisho kwa mabadilishano ya wachezaji Eric Lamela ambaye atakwenda Sevilla, huku Bryan Gil akielekea jijini London.

Mabadilishano hayo yanaelezwa yako ukingoni, huku wachezaji wote wawili wakiridhia na endapo Sevilla itapata saini ya Lamela basi watalipwa euro milioni 25 kutoka Spurs na kutakuwa na ada ya ziada.



Katika msimu huu Gil amecheza mechi 21 tu na amefunga mabao mawili na kutoa pasi mbili za mwisho.

Mchezaji huyo ana uwezo wa kucheza winga zote mbili pamoja na namba 10 na hivyo atakuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha Spurs.

Spurs wanajipanga kuimarisha kikosi chao baada ya kutokuwa na msimu mzuri uliopita na lengo ni kurudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa upande wa Lamela amekuwa akihangaika sana kufanya vyema kwa misimu ya hivi karibuni, na ataondoka klabuni hapo akiwa amecheza mara 257 na kufunga mabao 37 na kutoa asisti 47.

## KWA UFUPI

### PSG WAMFUATA POGBA
KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba ananyatiwa na Paris St-Germain msimu huu wa joto na klabu hiyo ya Ligue 1 inapanga kuwauza wachezaji kadhaa kukusanya pauni milioni 50 wanazoamini zitafanikisha azma ya kumsajili. ***(Mirror)***

### UNITED YASHANGAA
MANCHESTER United hawajapokea ofa yoyote kutoka PSG kuhusu uwezekanao wa uhamisho wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliye na umri wa miaka 28, Paul Pogba. (Manchester Evening News)

### NYOTA BARCA KUUZWA
BARCELONA wanajiandaa kuuza wachezaji ili kufadhili mkataba wa mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, kabla ya msimu mpya kuanza. ***(Guardian)***

### VARANE NJIA MOJA
MLINZI wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane, mwenye umri wa miaka 28, ana matumaini uhamisho wake kwenda Manchester United utakamilishwa siku chache zijazo. ***(AS)***

### ARSENAL WAMPANIA LOCATELLI
WAKALA wa kiungo wa kati wa Juventus, Nicolo Fagioli mwenye umri wa miaka 20 ambaye ni sehemu ya mkataba wa kubadilishana mchezaji wa Sassuolo, Manuel Locatelli - amethibitisha Arsenal wamewasilisha dau la pauni milioni 34 kutaka kumsajili nyota huyo. ***(Sky Italy, via London Evening Standard)***

### MADDISON KUMTOA NELSON
ARSENAL wapo tayari kuipatia Leicester City wachezaji kadhaa - akiwamo winga Reiss Nelson mwenye umri wa miaka 21 kama sehemu ya mkataba wa kumsaini kiungo wa kati wa England, James Maddison mwenye umri wa miaka 24. ***(Daily Mail)***

### NETO ANUKIA ARSENAL
ARSENAL wameimarisha juhudi zao za kuwania kumsajili golikipa wa Barcelona, Neto mwenye umri wa miaka 31. ***(Mundo Deportivo, via The Sun)***

### HAALAND DAU JUU
CHELSEA huenda wakawasilisha dau la pauni milioni 135 ili kumsajili Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(ESPN, via 90 min)***

### GIL AKARIBIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inakaribia kufikia makubaliano na winga wa Sevilla, Bryan Gil ambapo utamwezesha mshambuliaji wa Argentina, Erik Lamela kuhamia klabu hiyo ya LaLiga. ***(Sky Sports)***

### UNITED KUSAJILI WAWILI
MANCHESTER United wana nafasi ya kuwasajili wachezaji wawili kabla ya dirisha la uhamisho wa wachezaji kufungwa ndani ya wiki sita. Beki wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa. ***(Manchester Evening News)***

### ICARDI KUMPISHA RONALDO
JUVENTUS wanatathmini uwezekano wa mkataba wa kubadilishana wachezaji ambao utamwezesha Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, kujiunga na PSG nao wampate mshambuliaji wa Argentina, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 28. ***(L'Equipe via Daily Star)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI AMTAKA MBAPPE AU SALAH

**●●●Lengo ni kuimarisha safu yake ya ushambuliaji ambayo kwa sasa iko chini...**

**MADRID, Hispania**

KOCHA mpya wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, ameutaka uongozi wa klabu hiyo kumpatia Kylian Mbappe au Mohamed Salah kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Hispania, kwa mujibu wa Marca.

Mambo yanaonekana kuwa magumu wakati huu wa usajili wa kipindi cha majira ya joto kwa Real Madrid ambapo bado hawajafanya usajili wowote wa maana.

Tayari wamempoteza nahodha wao, Sergio Ramos ambaye ametua kwa miamba ya Ligi Kuu Ufaransa, PSG.

Huku kiungo wake, Eden Hazard akionekana 'tia maji tia maji', Ancelotti sasa anataka Madrid imsajili Mbappe kutoka PSG au Salah wa Liverpool.

Kwa mujibu wa ripoti, klabu hiyo ya dimba la Santiago Barnabeu inafuatilia kwa makini sakata la Mbappe kule PSG linavyokwenda.

Mbappe mwenyewe hadi sasa ameigomea PSG kusaini mkataba mpya na anataka kuondoka akiwa huru mwaka 2022, huku klabu hiyo sasa inaangalia uwezekano wa kumuuza badala ya kumwachia huru akimaliza mkataba wake.

Madrid hawana wachezaji mahiri kwenye safu ya ushambuliaji kwa sasa ambapo pengine Ancelotti anawaona hao kama ndio wachezaji wa kutegemea kuelekea msimu ujao.

Kocha huyo anataka straika mmoja kwa ajili ya kumsaidia Karim Benzema ambaye ndiye pekee amebakia kama kiongozi kwenye safu ya ushambuliaji ya klabu hiyo kwa sasa.

Ripoti hiyo inasema kocha huyo raia wa Italia amemweleza wazi Rais wa Real Madrid, Florentino Perez kuwa anataka nyota mpya atue Bernabeu kwenye usajili wa majira haya.

Katika hili, Ancelotti amemtaja Salah kama mchezaji anayemhitaji endapo itashindikana kwa Mbappe kutua Madrid wakati huu.

Inasemekana Salah ameshawaeleza Liverpool mara kadhaa kuwa anataka kwenda Madrid na pia, mahusiano yake na Jurgen Klopp na baadhi ya wachezaji wa Liverpool sio mazuri kwa sasa.

Linapokuja suala la gharama, Salah hatajwi kama mchezaji wa gharama kubwa akilinganishwa na Mbappe, lakini kwa vyovyote Madrid lazima wauze wachezaji ili wafanikishe mchakato wa kumsajili mchezaji wa kariba ya Mbappe au Salah.

## HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAKANUSHA KUACHANA NA CHIRWA

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiwa katika mchakato wa kuimarisha kikosi chake kwa kusajili wachezaji nyota kutoka sehemu mbalimbali, uongozi wa Azam FC umesema bado haujaachana na mshambuliaji wake raia wa Zambia, Obrey Chirwa.

Azam FC imelazimika kutoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa taarifa za kuachwa kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga pamoja na Mghana Yakubu Mohammed, Ally Niyonzima na Mkongomani Mopiana Mozinzi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema muda ukifika na kwa kufuata taratibu, klabu hiyo itatangaza wachezaji itakaowaacha baada ya kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi.

Popat alisema wanahitaji kuwa na kikosi imara kwa ajili ya msimu ujao, hivyo mchakato wa kusajili kikosi kipya wanaufanya kwa umakini zaidi.

"Ni kweli ukisajili ni lazima baadhi ya wachezaji waondoke, lakini mpaka sasa Azam FC bado hatujatangaza mchezaji tuliyemwacha," alisema Popat.

Tayari Azam FC imeshawasajili wachezaji wawili wa kigeni ambao ni Wazambia, Rodgers Kola akitoka katika klabu ya Zanaco pamoja na Charles Zulu aliyekuwa akichezea klabu ya Cape Town City ya Afrika Kusini.

Nyota mwingine aliyesajiliwa katika kikosi hicho kilichomaliza msimu uliopita kwenye nafasi ya tatu ni beki wa kushoto, Edward Charles kutoka Ruvu Shooting ya Mlandizi mkoani Pwani.

Azam iliyomaliza nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu, itashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho msimu ujao ambapo kwa mujibu wa kalenda ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), michuano hiyo itaanza mapema Septemba.

Timu nyingine zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa mwakani ni pamoja na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Yanga iliyomaliza ya pili na Biashara United kutoka Musoma mkoani Mara.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kulia), akibadilishana nakala za mkataba na mshambuliaji, Keneth Muguna kutoka Gor Mahia ya Kenya baada ya kumsajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

# Kampuni tatu zaitamani Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kampuni ya simu za mikononi, Vodacom kujiondoka kudhamini Ligi Kuu Tanzania Bara, kampuni tatu zinatajwa kuanza mazungumzo kwa ajili ya kuidhamini ligi hiyo, imefahamika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, aliliambia gazeti hili wanaishukuru Vodacom kwa muda wote waliodhamini ligi hiyo na kuongeza mchango wao umesaidia kulinyanyua soka la hapa nchini.

Hata hivyo, Kasongo hakuwa tayari kutaja kampuni hizo ambazo zinawania kudhamini ligi hiyo kwa msimu ujao utakaokuwa na timu 16.

"Vodacom wamemaliza mkataba wa kuidhamini ligi yetu, tunawashukuru kwa muda wote tuliokuwa nao, walitushika mkono kwa takribani miaka 20 kuanzia mwaka 2002. Kuna kampuni tatu, moja la ndani na mbili kutoka nje ya nchi, tunaendelea na mazungumzo nayo vizuri," Kasongo alisema.

Kiongozi huyo alisema wanaamini mdhamini mpya watakayempata atasaini donge nono zaidi na hii itasaidia kuongeza ushindani kwa timu zote zitakazoshiriki.

"Kwa kuwa mtoto (Ligi Kuu) anakua, hivyo dau pia nalo litakuwa kubwa zaidi, hivyo tusubiri muda ufike mambo yatakuwa hadharani," Kasongo alisema.

Tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeshaingia mkataba wa miaka 10 kwa ajili ya kudhamini ligi hiyo na Azam Media wenye thamani ya Sh. bilioni 225.

## Kagera yahitaji wachezaji nane

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuinusuru timu katika janga la kushuka daraja, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, ameweka wazi anahitaji kusajili wachezaji nane wapya ili kuimarisha kikosi chake kuelekea katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kagera Sugar iliyojikusanyi pointi 40 ilimaliza msimu uliopita ikiwa katika nafasi ya 12, ambayo ni ya mwisho huku timu zilizofuatia, Mtibwa Sugar na Coastal Union zikiangukia kucheza mechi za mchujo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema anahitaji kuongeza nguvu katika kikosi chake na ili kuwa imara atasajili wachezaji wasiopungua nane kwa kuzingatia nafasi mbalimbali alizopendekeza.

Baraza alitaja nafasi hizo ambazo anataka kuziboresha ni pamoja na beki wa pembeni, beki wa kati, kiugo mkabaji, mshambuliaji mmoja wa pembeni na washambuliaji halisi wawili.

"Nahitaji kuimarisha hizo nafasi, kesho (leo) nitakutana na viongozi wangu kwa ajili ya kuwapa ripoti ya awali na mwisho wa wiki hii nitakabidhi ripoti kamili kuhusu mikakati yangu kuelekea msimu mpya," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema kikao cha leo, hakitaonyesha usajili ila kitatoa mwongozo wa mahitaji muhimu ya timu hiyo ikiwamo programu za maandalizi ya msimu ujao na kuhakikisha hawarudii makosa yaliyojitokeza katika msimu uliomalizika.

## Dodoma Jiji FC yaanza mipango

**Na Shufaa Lyimo**

HAKUNA kulala! Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Makata, amesema wiki ijayo anatarajia kukabidhi ripoti yake ya msimu huu ambayo ameambatanisha na aina ya wachezaji ambao anawaohitaji ndani ya kikosi hicho.


Akizungumza na gazeti hili jana, Makata alisema msimu uliomalizika ulikuwa na ushindani mkubwa na anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na hatimaye wataendelea kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Ninatarajia kuanza zoezi la usajili wiki jayo baada ya kuikabidhi ripoti yangu, lengo ni kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani kwenye kikosi changu msimu ujao na hatimaye kufikia malengo," alisema Makata.

Kocha huyo alisema kuna baadhi ya wachezaji ambao mikataba yao imemalizika atajaribu kuzungumza nao ili kuwaongeza mikataba au kuwaruhusu kwenda kujiunga na klabu nyingine endapo watashindwa kufikia makubaliano.

"Kuna wachezaji ambao ninawahitaji nitahakikisha ninawabakiza, kikubwa ninahitaji kuwa na kikosi chenye ubora zaidi kuelekea msimu ujao," alisisitiza kocha huyo.

Michezo
Alhamisi Julai 22, 2021
Nipashe



## Ancelotti amtaka Mbappe au Salah

HABARI UK. 22



Kiungo wa Simba, Clatous Chama akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Yanga itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma. **PICHA: SIMBA SC**

## Coastal yashikwa Mtibwa yatakata

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Muungano Tanzania mwaka 1990, Pamba ya Mwanza, walishindwa kutumia vyema Uwanja wa Nyamagana, walipolazimishwa sare ya mabao 2-2 na wageni Coastal Union katika mechi ya kwanza ya mchujo, kusaka timu itakayocheza Ligi Kuu msimu wa 2021/22.

Abdallah Suleiman 'Sopu' aliifungia Coastal Union bao la kwanza sekunde ya 19 kabla ya James Ambrose kuisawazisha Pamba dakika ya 11 na kufanya timu hizo kwenda mapumziko wakiwa sare ya goli 1-1.

Bao la pili la Pamba lilifungwa na Emmanuel Haule kwa penalti wakati Raizin Hafidhi aliisawazishia Coastal Union dakika tatu kabla ya mechi kumalizika.

**Kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Hamadi Hilika alifunga ma bao matatu maarufu kama 'hat-trick', Mtibwa Sugar ikiichapa Transit Camp ya Dar es Salaam mabao 4-1, kwenye mechi nyingine ya 'play off'.**

Kelvin Sabato alifunga pia bao lingine kwa Mtibwa na Karegea Hazanga aliifungia bao la kufutia machozi, Transit Camp.

Hatima ya Coastal Union na Mtibwa Sugar kama zitabaki Ligi Kuu au kuteremka daraja, zitajulikana keshokutwa baada ya mechi za marudiano.

# SIMBA YATAMBA IMEPATA 'DAWA'

## ●●●Ni katika kuelekea mchezo wa watani huku Yanga ikiwaambia...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba Mfaransa Didier Gomes amesema ameshapata 'dawa' ya kuondoka na ushindi katika mechi ya fainali ya Kombe la FA, uongozi wa Yanga wenyewe umeweka wazi kikosi chao kiko imara kuhakikisha wanaendeleza ubabe dhidi ya watani zao.

Simba na Yanga zinatarajia kukutana katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gomes alisema kwa kushirikiana na benchi lake la ufundi amepata muda wa 'kuisoma' na kuipeleleza Yanga na kuweka mipango ya kuwamaliza.

Gomes alisema kikosi chake kimeshabaini mahali walipokosea, hivyo kamwe hawatarudia kosa hilo kwa ajili ya kuhakikisha wanatetea ubingwa wa michuano hiyo ambao wanaushikilia.

"Tumepata muda wa kukaa na kupitia mkanda wa video ya mchezo uliopita dhidi ya Yanga na kubaini upungufu na ubora wa wapinzania wetu, lakini tumeangalia na mechi zao nyingine kwa ajili ya kupunguza na kujiimarisha kwa kuangalia makosa yao," alisema Gomes.

Aliongeza wamejipanga kuhakikisha wanafuta machungu ya kupoteza mchezo wao wa mwisho ambao walilala kwa bao 1-0.

"Katika mazingira yoyote, ninaahidi kuondoka na ushindi, tunakwenda kwenye fainali kulipa kisasi kwa Yanga," Gomes alisema.

Aliongeza lengo lao ni kuona wanamaliza msimu huu kwa heshima na kushinda mchezo huo ndio jambo pekee wanalosubiri kuona linatimia.

Alisema tayari ameshapata 'dawa ya kumaliza' Yanga ambao ni kutumia washambuliaji watatu kama alivyofanya katika dakika za mwisho za mchezo dhidi ya Namungo FC ambapo aliwatumia kwa pamoja washambuliaji wake watatu ambao ni Chris Mugalu, Meddie Kagere na nahodha John Bocco.

"Unajua kuwatumia Bocco, Mugalu na Kagere kwa pamoja maana yake ni mwendo wa kushambulia na kutaka kupata bao, kama ilivyo katika michezo miwili ya mwisho, tutakwenda na mfumo huo kwa sababu tunahitaji kutetea taji la FA," alisema Gomes.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, aliliambia gazeti hili wanaimani na kikosi chao na wamejiandaa kwenda kufunga msimu wa 2020/21 kwa kishindo.

"Viongozi tuna imani na wachezaji na benchi la ufundi katika kufikia malengo tuliyojiwekea msimu huu, tutaendelea kusajili wachezaji bora ili tufanye vizuri kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tutajiimarisha ili kufanikisha hilo na hapa nyumbani hizi 'back to back' zitakuwa nyingi sana," alisema Barbara.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz amesema timu yao iko imara na wanakwenda Kigoma kwa kazi moja ya kuchukua kikombe cha mashindano hayo.

Nugaz alisema wao wanahitaji ushindi ili kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa nguvu zao.

"Sisi tunajua kujiandaa kwa ajili ya kuifunga Simba, mechi ya FA imeshamalizika," Nugaz alisema kwa kifupi.

Wakati huo huo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara ameamua kuachana na klabu hiyo kwa kile alichosema amechoka 'kuandamwa'.

"Hivi vitimbi mnavyonifanyia kila siku kisa Simba vishanichosha, mwisho wa siku mtanitoa roho yangu kabla ya muda wangu. Imetosha kwa sasa," alisema Manara.

Katika hatua nyingine, mwamuzi kutoka Manyara, Ahmed Arajiga ameteuliwa kuchezesha mchezo huo wa watani wa jadi akishirikiana na Fredinand Chacha (Mwanza), Mohamed Mkono (Tanga) na Elly Sasii wa Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002